

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**HOTUBA YA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA
BITEKO (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
FEDHA KWA MWAKA 2020/2021**



DODOMA

APRILI, 2020



Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Waziri wa Madini akitoa hotuba wakati wa uzinduzi wa Soko la Kimataifa la Madini - Mwanza

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA
BITEKO (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
FEDHA KWA MWAKA 2020/2021**

VIONGOZI WA WIZARA



Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.)
Waziri wa Madini



Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.)
Naibu Waziri wa Madini



Prof. Simon Samwel Msanjila
Katibu Mkuu

YALIYOMO

A. UTANGULIZI.....	1
B. UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA MADINI KATIKA PATO LA TAIFA	10
C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020	11
I. MAPATO	11
II. MATUMIZI	12
III. VIPAUMBELE VYA WIZARA	13
IV. UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE	14
V. UTEKELEZAJI KATIKA MAENEKO MENGINE	30
KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA MADINI	46
I. TUME YA MADINI	47
II. TAASISI YA JILOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST) ..	53
III. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)	64
IV. TAASISI YA UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA (TEITI)	71
V. CHUO CHA MADINI	73
VI. KITUO CHA JIMOLOJIA TANZANIA (TGC)	79
D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021	83
KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021	91
I. TUME YA MADINI	91
II. TAASISI YA JILOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST) ..	93
III. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)	96
IV. TAASISI YA UHAMASISHAJI UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA (TEITI)	98
V. CHUO CHA MADINI (MRI)	98
VI. KITUO CHA JIMOLOJIA TANZANIA (TGC)	100
E. SHUKRANI.....	101
F. HITIMISHO.....	105
VIAMBATISHO	107

ORODHA YA MAJEDWALI

Na.	Maelezo ya Jedwali	Namba ya Jedwali
(a)	Makadirio na Makusanyo Halisi ya Maduhuli kwa Kila Kituo kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na Makadirio kwa Mwaka 2020/2021	1.
(b)	Kiasi cha Mrabaha na ada ya ukaguzi kilichokusanywa kutoka kwene madini mbalimbali kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi Februari, 2020	2.
(c)	Mwenendo wa Mauzo na Mapato ya Dhahabu katika Masoko ya Geita, Chunya na Kahama kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020	3.
(d)	Takwimu za Mitambo ya Uchenjuaji Dhahabu Nchini mpaka Machi, 2020	4.
(e)	Takwimu za maendeleo ya Taaluma kwa Wahitimu wa Mwaka wa Masomo 2018/19 katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI)	5.
(f)	Matetemeko makubwa yaliyotokea kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020	6.

ORODHA YA PICHA

Na.	Maelezo ya Picha	Namba ya Picha
(a)	Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakibadilishana mawazo na Viongozi wa Wizara ya Madini	1
(b)	Wananchi wa Bukombe wakimsikiliza Mbunge wao Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko katika moja ya ziara zake	2
(c)	Soko Kuu la Dhahabu Chato (kulia) na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (<i>kushoto</i>) wakifurahia Madini ya Dhahabu baada ya kutembelea Soko la Dhahabu Geita katika moja ya ziara zao kukagua shughuli za madini	3
(d)	Muonekano wa cheti cha ICGLR	4
(e)	Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Waziri wa Madini akitoa Leseni ya Uchimbaji Madini kwa mmoja wa Wawakilishi wa Vikundi vya Wachimbaji Wadogo	5
(f)	Mh. Stanslaus Nyongo Naibu Waziri wa Madini akiwasilisha mada katika maonesho ya Indaba (Mining Indaba 2020 Conference) yaliyofanyika Afrika Kusini kuanzia tarehe 02 hadi 06 Februari, 2020	6
(g)	Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifunga Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini 2020	7
(h)	Baadhi ya Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Watumishi wa Wizara ya Madini wakishiriki katika Semina ya Udhhibit wa Rasilimali Madini	8

(i)	Baadhi ya Vituo vya Umahiri kati ya Vituo Saba Vilivyojengwa katika Mikoa Mbalimbali Nchini	9
(j)	Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Naibu Waziri wa Madini akishuhudia zoezi la uthaminishaji Madini ya Almasi katika Mnada wa Almasi Mwadui - Shinyanga	10
(k)	Mhe. Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Tukio la Utiaji Saini wa Mkaabata Kati ya Serikali na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Barrick wa kuanzishwa kwa Kampuni ya Ubria ya Twiga Minerals Corporation Limited	11
(l)	Mh. Stanslaus Nyongo Naibu Waziri wa Madini (Kushoto) na Prof. Simon Msanjila Katibu Mkuu wa Madini (kulia) kwa nyakati tofauti wakishiriki katika Kipindi cha Jambo Tanzania (TBC1) ikiwa ni sehemu ya kampeni ya kuelimisha Umma ya 'Madini Yatatutoa'	12
(m)	Muonekano wa Mfumo wa Ulinzi wa CCTV kamera, Jengo la Kituo cha Pamoja na Ukuta Kuzunguka machimbo ya Tanzanite Mirerani - Manyara	13
(n)	Timu ya Wakaguzi ikiwa katika Ukaguzi wa Mgodi	14
(o)	Wajijolojia wakichunguza na kukusanya takwimu kuhusu miamba katika eneo la QDS 293 lililopo Nachingwea mkoani Lindi	15
(p)	Katibu Mkuu Wizara ya Madini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilano (Uchukuzi) wakiwa katika ziara ya kukagua uwepo wa madini katika eneo la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR)	16
(q)	Wataalam wa Maabara ya GST Wakifanya Uchunguzi wa Sampuli	17
(r)	Vyungu vya kuyeyushia dhahabu (crucibles) na	18

	Cupels mara baada ya kutengenezwa katika maabara ya GST	
(s)	Mtambo wa kuchenjua dhahabu katika Mgodi wa STAMIGOLD	19
(t)	Mchoro Wa Kitakachokuwa Kiwanda Cha Kusafisha Dhahabu Jijini Mwanza	20
(u)	Wataalam wa STAMICO wakiwa katika Shughuli za Uchorongaji	21
(v)	Wanafunzi wa Chuo cha Madini wakifanya mafunzo kwa vitendo mgodini.	22
(w)	Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa pamoja wakitia saini hati ya makubaliano (MoU) kuhusu Chuo cha Madini kulelewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	23
(x)	Wanafunzi wa Kituo cha TGC wakiwa katika mafunzo ya uongezaji thamani madini	24
(y)	Vinyago Vilivyotengenezwa kwa mawe na Kituo cha TGC Arusha kwa ajili ya Mapambo ya Nyumbani na Ofisini	25

ORODHA YA VIELELEZO

Na.	Aina ya Kielelezo	Namba ya Kielelezo
(a)	Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020	1.
(b)	Makusanyo ya maduhuli kwa vyanzo mbalimbali kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020	2.
(c)	Kiasi cha dhahabu kilichozalishwa katika migodi mikubwa na kuuzwa nje ya nchi, mwaka 2013 - 2019	3.
(d)	Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Madini ya Dhahabu katika Soko la Dunia kuanzia mwaka 2007 - 2019	4.
(e)	Ramani inayoonesha vituo vyatupu kupimia mitetemo ya ardhi	5.

ORODHA YA VIFUPISHO

ADPA	African Diamonds Producers Association
BLs	Brokers Licences
CAG	Controller and Auditor General
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CCTV	Closed Circuit Television
CSR	Corporate Social Responsibility
Dkt.	Daktari
DLs	Dealers Licences
ERB	Engineers Registration Board
GDP	Gross Domestic Product
GePG	Government e-Payment Gateway
GMIS	Geological Mineral Information System
GST	Geological Survey of Tanzania
ICGLR	International Conference on the Great Lakes Region
ICT	Information and Communications Technology
KPCS	Kimberly Process Certification Scheme
Mb.	Mbunge
MKURABITA	Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania
MLs	Mining Licences
MoU	Memorandum of Understanding
MRI	Mineral Resources Institute
MROs	Mines Resident Officers
MSY	Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza
NEMC	National Environment Management Council
OC	Other Charges
OPRAS	Open Performance Review and Appraisal System
PCLs	Processing Licences
PDAC	Prospectors and Developers Association of Canada
PLs	Prospecting Licences
PMLs	Primary Mining Licences
QDS	Quarter Degree Sheet
REE	Rare Earth Element
REPOA	Research on Poverty Alleviation
RFL	Refiner Licence
SADC	Southern African Development Community
SADCAS	Southern African Development Community Accreditation Service

SDGs	Sustainable Development Goals
SGR	Standard Gauge Railway
SL	Smelting License
SMMRP	Sustainable Management of Mineral Resources Project
STAMICO	State Mining Corporation
TBC	Tanzania Broadcasting Corporation
TEHAMА	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TEITA	Tanzania Extractive Industries Transparency Accountability Act
TEITI	Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative
TGC	Tanzania Gemmological Centre
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
WDL	Williamson Diamonds Limited
XRF	X-Ray Fluorescence

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA
BITEKO (MB.), WAZIRI WA MADINI
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA
MWAKA WA 2020/2021**

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Madini, Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka wa 2019/2020 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2020/2021.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kwa mara nyingine kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 mbele ya Bunge lako Tukufu.

3. **Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Madini. Napenda kutoa pongezi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini na thabiti. Mafanikio hayo yanajidhihirisha katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa ya maendeleo ikiwamo Mradi wa Ufuaji Umeme wa Bonde la Mto Rufiji (Julius Nyerere Hydro power project), ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway), ununuzi wa ndege mpya kufufua Shirika la Ndege Tanzania na miradi mingine kadhaa.

4. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio hayo ya Kitaifa, nimshukuru tena Mheshimiwa Rais, kwa hatua madhubuti alizochukua yeze binafsi katika kuzilinda rasilimali madini na kuhakikisha kuwa zinawanufaisha wananchi hasa wanyonge na kulinda maslahi ya Taifa. Watanzania watakuwa ni mashahidi wa mafanikio hayo kama ifuatavyo:

(i) *Uanzishwaji wa Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited*

5. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mara ya kwanza chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais, Serikali ya Tanzania imeingia ubia na Kampuni ya Barrick Gold Corporation na kuanzisha Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited. Uwekezaji huu unaipa Serikali umiliki wa hisa asilimia 16 na Kampuni ya Barrick Gold

Corporation umiliki wa hisa asimilia 84. Katika makubaliano hayo imekubaliwa pia kwamba kutakuwa na mgawanyo wa manufaa ya kiuchumi ya 50:50 hii ikiwa na maana ya kwamba faida na mapato mengine nje ya uendeshaji kuondolewa itatakiwa kuwekezwa nchini kiasi kisichopungua asilimia 50. Hatua hii itasaidia kulinda maslahi mapana ya nchi na kuongeza udhibiti katika shughuli za uzalishaji madini. Kipekee kabisa nikiri, uthubutu wa namna hii uliwahi kufanyika wakati wa Uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Serikali ilipokuwa na ubia na Kampuni ya Williamson Diamond Limited (WDL). Hakika uongozi wake ni Tunu kwa Taifa.

(ii) Uanzishaji na Usimamizi wa Masoko nchini

6. **Mheshimiwa Spika,** nashawishika kusema maono ya Mheshimiwa Rais ni baraka kwa Watanzania, kwa dhamira yake tumeweza kuanzisha masoko na vituo vyta ununuzi wa madini katika maeneo mbalimbali yenyе shughuli za uchimbaji madini nchini. Nikiri kuwa, Masoko haya yamesaidia kutatua changamoto za muda mrefu ambazo zilikuwa zikiikabili Sekta ya Madini hususan wachimbaji wadogo kukosa masoko ya uhakika na bei stahiki ambapo katika kipindi cha kuanzia Machi 2019 hadi Februari 2020 kupitia masoko wachimbaji wadogo wamefanya biashara ya madini yenyе thamani ya shilingi **1,088,693,000,153.19** na wameiingizia Serikali

mapato kwa kulipa mrabaha na ada ya ukaguzi wa **shilingi 78,008,413,233.13**. Masoko haya yameleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa Sekta hii kwa kipindi cha Januari hadi Septemba iliongezeka kutoka asilimia 0.9 mwaka 2018 hadi asilimia 12.6 mwaka 2019 kwa kipindi kama hicho. Masoko hayo yameleta manufaa mengine kwa wananchi ikiwemo kuzalisha fursa za ajira na kuongezeka kwa kipato cha wachimbaji wadogo tofauti na hapo awali. Namuomba Mungu azidi kumjalia maono zaidi na zaidi ili Watanzania wazidi kuneemeka.

(iii) Uanzishwaji wa Eneo Tengefu la Mirerani

7. ***Mheshimiwa Spika***, katika namna isiyokuwa rahisi kuaminika katika macho ya wengi, pale neno la Mungu lilipomjia Mheshimiwa Rais hakutaka kukimbia wito kama "Yona mwana wa Amitai, kwenda Ninawi", amekamilisha ujenzi wa Ukuta kuzunguka machimbo ya madini eneo la Mirerani na kuweka vifaa vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha kuwa madini ya Tanzanite ambayo ni rasilimali ipatikanayo Tanzania pekee inalindwa. Kufuatia uwekezaji huo, sote tumeshuhudia kuongezeka mara dufu kwa mapato yatokanayo na madini ya Tanzaite katika eneo hilo hususan kutoka kwa wachimbaji wadogo kutoka **shilingi 166,094,043** kabla ya

kujenga ukuta hadi **shilingi 2,150,000,000** baada ya kujengwa kwa ukuta. Kipekee namuomba Mungu azidi kusema nae.

(iv) Uendelezaji wa Uchimbaji Mdogo Nchini

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa azma ileile ya kutetea haki za wanyonge, Mheshimiwa Rais alifuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi ya Zui o kwa wachimbaji wadogo hii ikiwa ni huruma yake kwa wachimbaji wadogo na mkakati wake wa kuhamasisha uendelezaji wa uchimbaji mdogo nchini. **Nitoe rai kwa wachimbaji wadogo kuunga mkono juhudzi za Uongozi Shupavu wa Awamu ya Tano kwa kuhakikisha wanatumia fursa hiyo ili kujinufaisha na rasilimali madini ambazo nchi yetu imejaliwa.**

9. **Mheshimiwa Spika**, nikiri kuwa, sio siri kuwa Mheshimiwa Rais ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa chini ya uongozi wake maendeleo ya Taifa letu yanaonekana kila mahali. Nawiwa kusema hakika mioyo ya watanzania inamwombea afya njema ili aendelee kuliongoza Taifa hili kuelekea *Nchi ya Ahadi ya Maziwa na Asali*. Hakika historia imeandikwa na itaendelea kukumbukwa na kizazi hiki na kijacho.

10. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati ninapenda kumshukuru Mheshimiwa **Samia Suluju**

Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi makini na miongozo mbalimbali ambayo amekuwa akitupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu. Vilevile, nimshukuru Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa** (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Bunge lako Tukufu. Pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya kusimamia Sekta ya Madini nchini.

11. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambazo limefanya katika kipindi cha uongozi wako. Aidha, ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa katika kipindi chote cha Bunge la 11. Ni dhahiri kuwa, Bunge hili limefanya kazi ya kutukuka ya kuisimamia na kuishauri Serikali pamoja na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Chini ya uongozi wako mahiri, Bunge limeweza kupitisha Sheria mbalimbali ikiwemo Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 ambayo yamesaidia katika

kuimarisha na kukuza Sekta ya Madini na kuiwezesha kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Marekebisho haya yamewafanya Watanzania waweze kunufaika na rasilimali madini ambazo Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa.

12. **Mheshimiwa Spika**, naishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Dustan Luka Kitandula (Mb.), Mheshimiwa Mariamu Ditopile Mzuzuri (Mb.) Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri mzuri walionipatia katika kipindi chote cha mwaka 2019/2020. Aidha, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka 2019/2020; na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2020/2021. Ushauri, maoni na maelekezo ya Kamati vimesaidia katika kuboresha Mpango na Bajeti inayowasilishwa leo. Nikiri kuwa, mafanikio makubwa ya Sekta ya Madini yamechangiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na michango na miongozo inayotolewa na Kamati hii.



Picha Na. 1: Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakibadilishana mawazo na Viongozi wa Wizara ya Madini

13. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru Wabunge wote kwa ujumla wao kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutupatia ushauri kwa nyakati tofauti katika kipindi chote cha Bunge la 11. Hakika wamefanya kazi nzuri ya kuwawakilisha wananchi na kuisimamia Serikali kwa kuhakikisha maslahi mapana ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla yamezingatiwa.

14. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini kwa kifo cha Mheshimiwa Ajali Rashid

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kilichotokea tarehe 15 Januari, 2020. Aidha, ninatoa pole za dhati kwa wananchi waliopoteza ndugu na mali zao kutokana na ajali, maradhi na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Ninaomba Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

15. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Madini, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb), Naibu Waziri na Profesa Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu, Mhandisi David Mulabwa, Kamishna wa Madini na viongozi wengine wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kufanikisha majukumu yangu.

16. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa kuendelea kuniunga mkono na kunipa ushirikiano katika kutekeleza shughuli za maendeleo jimboni kwa ufanisi. Nawashukuru sana.



Picha Na. 2: Wananchi wa Bukombe wakimsikiliza Mbunge wao Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko katika moja ya ziara zake

17. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusini ya hotuba hii ambayo ni: Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa; Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka 2019/2020; Kazi zilizotekelizwa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2019/2020; na Mpango na Bajeti, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

B. UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA MADINI KATIKA PATO LA TAIFA

18. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa, katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2019 kasi ya ukuaji

wa Sekta ya Madini ulifikia asilimia **12.6**. Ukuaji huu uliifanya Sekta ya Madini kushika nafasi ya pili ikitanguliwa na Sekta ya Ujenzi iliyokua kwa asilimia **14.8**. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini mbalimbali yakiwamo dhahabu, makaa ya mawe, tanzanite na almasi.

19. ***Mheshimiwa Spika***, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa (GDP) umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka kutohana na ongezeko la kasi ya ukuaji wa sekta ikilinganishwa na sekta nyingine za kiuchumi. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2019 mchango wa Sekta katika Pato la Taifa ulifikia **asilimia 4.7**.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020

I. Mapato

20. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 476,380,613,492**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 470,897,011,000** zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina ambapo hadi kufikia Machi, 2020 **shilingi 358,870,785,797** zimekusanywa na kuwasilishwa Hazina. Makusanyo hayo ni sawa na **asilimia 102** ya lengo la **shilingi 353,172,758,250** katika kipindi husika. Aidha,

Taasisi zilizo chini ya Wizara zilipangisha kukusanya **shilingi 5,483,602,492.00** kwa matumizi ya Taasisi hizo. Hadi kufikia Machi, 2020 Taasisi zilikusanya jumla ya **shilingi 4,624,906,145.34** ambazo ni sawa na **asilimia 112** ya lengo la **shilingi 4,142,379,369** katika kipindi husika.

II. Matumizi

21. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka 2019/2020, Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya **shilingi 49,466,898,200.00**. Bajeti hii inajumuisha **shilingi 42,427,088,000.00** sawa na **asilimia 85.77** ya bajeti yote kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 7,039,810,200.00** sawa na **asilimia 14.23** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

22. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida, **shilingi 25,953,263,000.00** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **shilingi 16,473,825,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Kwa upande wa Fedha za Maendeleo kiasi chote cha **shilingi 7,039,810,200.00** ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) na Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI).

23. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 2020 Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa ni **shilingi 31,440,490,478**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 12,085,773,578 sawa na asilimia 38.44** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **shilingi 19,354,716,900 sawa na asilimia 61.56** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zake.

24. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Wizara iliendelea na utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kutumia kiasi cha **shilingi 6,197,175,564.39** ambazo zilizopokelewa mwaka wa fedha wa nyuma kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Mirerani, usimikaji wa Mfumo wa Ulinzi na Kamera za Usalama pamoja na miundombinu ya umeme kuzunguka ukuta wa eneo Tengefu la Mirerani.

III. Vipaumbele vya Wizara

25. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Madini ilikuwa na vipaumbele vifuatavyo: kuhimiza utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini; kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; uanzishwaji na usimamizi wa masoko ya madini; kudhibiti utoroshaji wa madini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa

kati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarissha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini; na kuendeleza rasilimaliwatu katika Wizara pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

IV. Utekelezaji wa Vipaumbele

(a) Kuimarissha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini

26. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara ya Madini ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya **shilingi 470,897,011,000** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hadi kufikia Machi, 2020 jumla ya **shilingi 358,870,785,797** zimekusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali ambazo ni sawa na **asilimia 102** ya lengo la **shilingi 353,172,758,250** katika kipindi husika.

27. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na uanzishwaji na usimamizi mzuri wa masoko na vituo vyta ununuzi wa madini, pia juhudzi za Wizara kuendelea kudhibiti utoroshwaji wa madini nchini; kufanya ulinganishi na usimamizi wa bei elekezi za madini ya dhahabu na vito

kulingana na mwenendo wa bei ya dunia; na matumizi ya Mfumo wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali (GePG) ambao umerahisisha ulipaji wa tozo mbalimbali; vimechangia kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli.

(b) Uanzishwaji na Uimarishwaji wa Masoko ya Madini

28. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Februari, 2020 jumla ya Masoko ya Madini 28; na vituo vyatunuzi wa madini 28 vimeanzishwa na kuwezesha kutatua changamoto kubwa zilizokuwa zinaikabili Sekta ya Madini kwa kipindi kirefu, zikiwemo wachimbaji wadogo kukosa sehemu za kuuza madini yao na uwepo wa utoroshaji na biashara haramu ya madini. Changamoto hizo zimekuwa zinasababisha Serikali kukosa malipo stahiki ya tozo mbalimbali zinazotokana na shughuli za madini; kukosekana kwa bei stahiki za madini kwa wachimbaji wadogo; na kukosekana kwa takwimu za uzalishaji na mauzo ya madini kutoka kwa wachimbaji wadogo.



Picha Na. 3: Soko Kuu la Dhahabu Chato (kulia) na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (kushoto) wakifurahia Madini ya Dhahabu baada ya kutembelea Soko la Dhahabu Geita katika moja ya ziara zao kukagua shughuli za madini.

29. **Mheshimiwa Spika,** tangu kuanzishwa kwa masoko hayo mwezi Machi, 2019 hadi Februari, 2020 kiasi cha tani 10.33 za madini ya dhahabu; karati 13,685.74 za madini ya almasi; tani 20.10 za madini ya bati; tani 550.87 za madini ghafi ya vito; na karati 90,532.41 za madini mengine ya vito kiliuzwa kupitia masoko hayo ambapo katika kipindi cha kuanzia Machi 2019 hadi Februari 2020 kupitia masoko wachimbaji wadogo wamefanya biashara ya madini yenye thamani ya shilingi **1,088,693,000,153.19** na wameiingizia Serikali mapato kwa kulipa mrabaha na ada ya ukaguzi **shilingi 78,008,413,233.13.**

(c) Kudhibiti utoroshwaji wa madini

30. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha udhibiti dhidi ya utoroshwaji wa madini, Wizara imeendelea na mkakati wa kukabiliana na biashara haramu ya madini ambapo Wizara

kwa kushirikiana na Vyombo vyta Ulinzi na Usalama, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Viwanja vyta Ndege na Mamlaka ya Bandari Tanzania imeweza kufanya kaguzi kwa kutumia kikosi kazi katika viwanja vyta ndege, Bandari na mipaka ya nchi.

31. **Mheshimiwa Spika**, katika kaguzi hizo, madini yenye thamani ya **Dola za Marekani 3,210,976.35** na **shilingi 1,556,209,334.61** yalikamatwa katika maeneo ya Tunduru, Kyerwa, Mwanza, Mirerani, Holili, Babati, Hai, Dodoma, Nzega na Kahama. Kaguzi hizo zitaongeza tija na kukuza mchango wa sekta katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa. **Nitoe wito kwa wafanyabiashara na wadau wa Sekta ya Madini kwa ujumla kufanya shughuli zao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini.**

32. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuzuia na kudhibiti utoroshaji wa madini ili kuondokana kabisa na tatizo hili hapa nchini na hivyo kuwa na taswira chanya kuhusu biashara ya madini. Mikakati hiyo ni pamoja na: kuimarisha usimamizi kwenye maeneo yote ya uzalishaji katika migodi mikubwa na ya kati kwa kuanzisha ofisi za Maafisa Migodi Wakazi yaani *Mines Resident Officers* (MROs); kuweka wasimamizi katika maeneo ya viwanja vyta ndege na mipakani ili kudhibiti utoroshaji wa madini; kuendelea kuhamasisha wauzaji na wanunuvi kutumia Masoko ya Madini ambayo hutoa bei elekezi; na

kuendelea kutoa elimu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo zinazohusu Sekta ya Madini.

33. ***Mheshimiwa Spika***, ili kudhibiti biashara haramu na utoroshwaji wa madini ya *Tin*, *Tantalum* na *Tungsten* (3Ts), tarehe 27 Januari, 2020 Tanzania ilipatiwa ithibati ya kutoa cheti cha uasilia kwa madini hayo. Upatikanaji wa ithibati hiyo ulifuatia Wizara kukamilisha taratibu za utoaji wa cheti cha uasilia wa madini hayo kwa mujibu wa makubaliano ya nchi wanachama wa Ukanda wa Maziwa Makuu (International Conference on the Great Lakes Region-ICGLR). Uzinduzi wa cheti hicho ulifanyika tarehe 23 Februari, 2020 na ulifanywa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

 <p>THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA REPUBLIQUE UNIE DE TANZANIE</p> <p>MINISTRY OF MINERALS MINISTERE DES MINES</p> <p>THE MINING COMMISSION COMMISSION MINIERE</p> <p>ICGLR REGIONAL CERTIFICATE CERTIFICAT REGIONAL DE LA CIRGL</p> <p>This is to certify that Shipment No. _____ comprised of designated minerals _____ Il est certifié que la cargaison N° _____ comprend des minéraux désignés _____</p> <p>mined in _____ Region in the United Republic of Tanzania has been province de la République Unie de Tanzanie ont été _____ extraits à _____ commercialisés et traités conformément aux exigences de la CIRGL.</p> <p>Exporter's Name and Address: _____ Nom et adresse de l'exportateur: _____</p> <p>Buyer's Name and Address: _____ Nom et adresse de l'acheteur: _____</p> <p>Date of Shipment: Date d'expédition: _____</p> <p>Date of Expiry of Certificate: Date d'expiration du certificat: _____</p> <p>Transiting Through: Lieu de transit: _____</p> <p>Designated Mineral (s) Minéraux désignés</p> <p>Contained Metal(s) Contenu en métal</p> <p>Net Weight (kg) Poids net (kg)</p> <p>Purity (%) Pureté (%)</p> <p>Value (USD) Volume (USD)</p> <p>Total _____</p> <p>Name of Authorised Officer: Nom de l'agent habilité _____</p> <p>Position: Poste: _____</p> <p>Signature and Official Stamp: Signature et tampon officiel Date: _____</p> <p>Stamp of importing authority Tampon de l'autorité à l'importation To be returned to: The Executive Secretary, The Mining Commission, P.O. Box 2292, Dodoma, TANZANIA À retourner au: Secrétaire Exécutif Commission Minière B.P. 2292, DODOMA TANZANIE</p>		 <p>TZ 000 123</p> <p>INTERNATIONAL CONFERENCE ON THE GREAT LAKES REGION CONFÉRENCE INTERNATIONALE SUR LA RÉGION DES GRANDES LACS</p> <p></p> <p>TANZANIA</p> <p>This is to certify that the certified product was imported to _____ Il est certifié que le produit homologué était importé de _____</p> <p>(Country) (Pays)</p> <p>and the import has been checked and verified in compliance with all rules and regulations concerning the certificate of origin. et l'importation a été vérifiée conformément à tous les règlements concernant le certificat d'origine</p> <p></p> <p></p> <p></p> <p>TZ 000 123</p>
---	--	--

Picha Na 4: Muonekano wa cheti cha ICGLR

(d) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa Kati wa madini

34. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na juhudzi za kutoa elimu juu ya Sheria ya Madini Sura ya 123 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 kwa wachimbaji wadogo na wa kati pamoja na wadau wengine wa Sekta ya Madini. Katika kutekeleza hili, Wizara imetoea elimu hiyo kwa wachimbaji zaidi ya 1,500 kupitia Maonesho ya Pili ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika tarehe 19 hadi 30 Septemba, 2019 katika Mkoa wa Geita na kwenye mkutano wa madini uliofanyika Dar es Salaam, tarehe 22 Februari, 2020. Aidha, kuanzishwa kwa masoko ya madini kumewawezesha wachimbaji wadogo kuongeza kipato chao kwa kuuza madini yao kwa bei elekezi.

35. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliainisha na kugawa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuratibu utoaji wa leseni 11 zenye jumla ya hekta 54 za uchimbaji mdogo kwa vikundi kumi (10) vya wachimbaji wadogo Wilayani Nzega. Aidha, leseni 22 zilitolewa kwa vikundi 22 vya wachimbaji wadogo katika eneo la Bululu Wilaya ya Nyang'hwale zenye jumla ya hekta 71.94 na leseni 15 zenye jumla ya hekta 131.47 zilitolewa kwa Ushirika wa Wachimbaji wa Dhahabu Irasanero, Buhemba Mkoa wa Mara kutoka kwenye eneo la utafiti mkubwa linalomilikiwa na

Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). Vilevile, leseni 23 zenye jumla ya hekta 189.73 zilitolewa tarehe 28 Juni, 2019 na kukabidhiwa rasmi tarehe 5 Julai, 2019 kwa vikundi vyat wa chimbaji wadogo wa dhahabu wa Mwakitalyo Mkoa wa Shinyanga. Lengo la kutenga maeneo haya ni kuhakikisha kuwa wachimbaji wadogo wanapata maeneo ya kufanya shughuli zao kwa uhakika na kujipatia kipato kwa mujibu wa Sheria.



Picha Na.5: Mheshiwa Doto Mashaka Biteko, Waziri wa Madini akitoa Leseni ya Uchimbaji Madini kwa mmoja wa Wawakilishi wa Vikundi vyat wa Chimbaji Wadogo.

36. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na STAMICO na wadau wengine imekuwa ikiwaelimisha wachimbaji wadogo namna bora ya utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini ili kuwaongezea tija. Mpaka sasa jumla ya

wachimbaji 900 wamepata mafunzo hayo sambamba na kuwasambazia kitabu cha Mwongozo wa Wachimbaji wadogo kilichoandaliwa na Wizara kwa ajili yao. Pia, Serikali inaendelea kuziimarisha Taasisi hizi ili ziweze kuwasaidia zaidi wachimbaji na kuwaongeza uwezo wa kufanya shughuli zao za uchimbaji kwa ufanisi.

(e) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini

37. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini ya metali, viwandani, ujenzi na vito. Aidha, katika kipindi rejewa Wizara ilitoa leseni mbili (2) za uyeyushaji madini (Smelters) na leseni tatu (3) za usafishaji madini (Refinery).

(f) Kuimarisha Ufuatiliaji na Ugakuzi wa Usalama, Afya, Mazingira na Uzalishaji wa Madini Katika Migodi

38. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kufanya kaguzi za Usalama, Afya Mahali pa Kazi na Utunzaji wa Mazingira katika migodi mikubwa, ya kati na midogo. Katika kipindi rejewa, jumla ya migodi mikubwa mitano (5) ya *Pangea Minerals Ltd* (Buzwagi), *Bulyanhulu Gold Mine Ltd*, *North Mara Gold Mine Ltd*, *Geita Gold*

Mine Ltd pamoja na mgodi wa *Williamson Diamonds Ltd* ilikaguliwa.

39. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya migodi 11 ya uchimbaji wa kati ilikaguliwa. Ukaguzi huu ulifanyika katika migodi ya: Nsoromero Minerals Co-operative Society Ltd; Mara Mine Development Ltd; Nyamongo (T) Ltd; Nyamongo Gold Mine Ltd; P.Z. Gold Mining Co. Ltd; MMG Gold Ltd; CATA Mining Co. Ltd; Perfalbion Minerals Ltd; na ZEM (T) Co. Ltd iliyopo mkoani Mara. Pia, ukaguzi ulifanyika katika mgodi wa Sunshine Ltd uliopo katika Mkoa wa Songwe.

40. ***Mheshimiwa Spika***, pia, kaguzi hizo zilifanyika katika maeneo ya wachimbaji wadogo ikiwemo: Mgodi wa Sekenke One Mining Society, eneo la Mwakitalyo, Maeneo yanayozunguka Ziwa Manyara, Migodi ya Bati- Kyerwa, Mgodi wa Busolwa, Mgodi wa Dhahabu wa Nsangano na eneo la uchimbaji wa Tanzanite.

41. ***Mheshimiwa Spika***, Kaguzi hizo zilibaini uwepo wa maboresho ya mapungufu yaliyobainishwa katika kaguzi zilizotangulia. Hata hivyo, kaguzi zilibaini uendeshaji wa shughuli za madini usiozingatia Sheria na Kanuni hususan katika utunzaji wa mazingira ikiwemo: kutokuwa na Mpango wa Ufungaji Mgodi; kutokuwa na utaratibu wa utupaji mawe takaa; na mabwawa ya kuhifadhi topesumu yaliyoidhinishwa. Migodi

husika ilielekezwa kufanya marekebisho katika mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kaguzi hizo na ufuatiliaji unaendelea kuhakikisha kasoro hizo zinarekebishwa.

42. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu suala la kutunza mazingira, Wizara ilifanya Kongamano la usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira katika Sekta ya Madini. Kongamano hilo lilifanyika jijini Dodoma kuanzia tarehe 16 hadi 17 Desemba, 2019 na lilijumuisha taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, NEMC, GST, Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi. Kongamano hili lilihusisha pia makampuni ya madini ya wachimbaji wakubwa na wa kati, na washauri waelekezi wa masuala ya mazingira. Madhumuni ya kongamano hilo yalikuwa ni kujadili kwa pamoja changamoto za utunzaji wa mazingira katika Sekta ya Madini na namna ya kukabiliana nazo; Kuwaleta pamoja wadau wa Sekta ya Madini kwa maana ya Serikali na sekta binafsi; na kupeana uzoefu kuhusu utunzaji endelevu wa mazingira na ufungaji migodi.

(g) Kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini

43. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye Sekta ya Madini Ndani na Nje ya Nchi, kupitia ushiriki katika mikutano ya kimataifa ikiwemo Mkutano wa Kwanza wa Uchumi na Biashara uliofanyika China tarehe 26 Juni hadi 01 Julai, 2019; Mkutano wa 16 wa Kimberly Process Certification Scheme (KPCS) uliofanyika New Delhi, India tarehe 18 hadi 22 Novemba, 2019; Mkutano wa Sita wa Nchi za Afrika zinazozalisha Madini ya Almasi (ADPA) uliofanyika nchini Namibia tarehe 8 hadi 9 Julai, 2019 na Kikao cha Kamati cha Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR) kilichofanyika Burundi tarehe 1 hadi 4 Oktoba, 2019.

44. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya ziara ya mafunzo nchini Brazil yaliyohusu uchimbaji wa madini ya *Rare Earth Element (REE)* Februari, 2020 na kushiriki katika maonesho yaliyofanyika Afrika Kusini (Mining Indaba 2020 Conference) kuanzia tarehe 02 hadi 06 Februari, 2020 na maonesho yaliyofanyika Canada (PDAC 2020) tarehe 01 hadi 04 Machi, 2020. Wizara pamoja na Taasisi zake ilishiriki katika maonesho ya 39 ya Nchi Wanachama wa SADC yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 17 hadi 18 Agosti, 2019.



Picha Na. 6: Mh. Stanslaus Nyongo Naibu Waziri wa Madini akiwasilisha mada katika maonesho ya Indaba (Mining Indaba 2020 Conference) yaliyofanyika Afrika Kusini kuanzia tarehe 02 hadi 06 Februari, 2020.

45. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mikutano hiyo kutoa fursa za kubadilishana uzoefu katika masuala ya madini, pia imesaidia kukuza ushirikiano baina ya nchi wanachama na kuchochea uwekezaji katika Sekta ya Madini. Aidha, Wizara imeendelea na mazungumzo ya Makubaliano ya Awali ya Ushirikiano (MoU) na nchi za Namibia, Zimbabwe, India na Qatar katika kubadilishana uzoefu kwenye maeneo ya utafutaji, uchimbaji, uongezaji thamani madini na biashara ya madini.

46. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliandaa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta

ya Madini 2020 uliofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 22 hadi 23 Februari, 2020. Ujumbe wa mukutano huo ulikuwa ni "***Uwekezaji na Ushirikiano Endelevu katika Sekta ya Madini***". Mukutano huo uliambatana na siku tatu (3) za maonesho ya Sayansi na Teknolojia katika Sekta ya Madini ambapo Wachimbaji Wakubwa, wa Kati na Wadogo walishiriki katika kuonesha vifaa vyta uchimbaji madini na bidhaa zitokanazo na madini. Aidha, katika mukutano huo kulikuwa na mawasilisho ya mada mbalimbali ikiwemo jiolojia ya Tanzania, uwekezaji barani Afrika, uongezaji thamani madini, masoko ya madini na Mabadiliko ya Sheria ya Madini nchini ikilinganishwa na Sheria katika nchi zingine.

47. ***Mheshimiwa Spika*** katika ufungaji wa mukutano huo mgeni rasmi ***Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)*** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Cheti cha Uasilia kwa madini ya *Tin, Tungsten na Tantalum* (3Ts) kufuatia Tanzania kukamilisha vigezo vyta kupata idhibati ya kutoa cheti hicho. Mukutano huo ulihudhuriwa na nchi 11 Wanachama wa ICGLR pamoja na wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini.



Picha Na. 7: Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifunga Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini 2020

48. **Mheshimiwa Spika**, mbali ya mikutano huo wa kimataifa, Wizara pia ilishiriki katika maonesho ya teknolojia ya madini yaliyofanyika Geita tarehe 19 hadi 30 Septemba, 2019. Mikutano yote hii ni sehemu ya jitihada za Wizara kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini hapa nchini.
49. **Mheshimiwa Spika**, ziara, mikutano na makongamano hayo yaliyofanyika ndani na nje ya nchi yameleta matokeo chanya ikiwemo kupewa leseni za uchimbaji wa madini ya kinywe (Graphite) kwa kampuni tatu (3) ambazo ni za ubia kati ya watanzania na wageni (China); STAMICO imepata wawekezaji

wawili katika mradi wa kusafisha dhahabu wa Mwanza na mradi wa kuchimba dhahabu wa Buhemba; STAMICO imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Shirika la Madini la Indonesia PT TIMAH tarehe 17 Desemba, 2019 ya kuendeleza leseni za Madini na tayari wawakilishi wa Shirika hilo wameshatembelea maeneo ya leseni hizo; na mwezi Julai, 2019 GST ilisaini MoU na Taasisi ya Jiolojia ya China (China Geological Survey) kwa ajili ya kufanya tafiti za jiosayansi katika mikoa ya Shinyanga na Mbeya.

(h) Kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini

50. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha wamiliki wa leseni za uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini pamoja na wakandarasi wanawasilisha na kutekeleza mipango ya ushirikishwaji wa watanzania katika mnyororo wa uchumi wa madini (Local Content). Mpango huo ni pamoja na kuwataka wawekezaji hao kuweka kipaumbele katika matumizi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini, kuajiri watanzania na kuondoa tofauti kubwa ya mishahara kwa kazi zinazofanana na kufanywa na wageni na Watanzania.

51. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Wizara ilipitia na kuidhinisha Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika utoaji wa huduma mbalimbali katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini kutoka kampuni 20 kati ya kampuni 76 zilizowasilisha ili zipatiwe leseni za madini. Sababu zilizosababisha kampuni 56 kukosa sifa za kuidhinishiwa mipango iliyowasilishwa ni pamoja na kutowasilisha kiapo cha uadilifu (Integrity Pledge); uhawilishaji wa teknolojia; kushindwa kuwasilisha bajeti ya utafiti na maendeleo; na kutokuwasilisha mpango wa mafunzo. **Napenda kuchukua nafasi hii kuyahimiza makampuni yote yanayoomba leseni za madini kuzingatia Sheria na Kanuni za utoaji leseni ikiwa ni pamoja na kuwasilisha Mpango wa Ushirikishwaji Watanzania unaokidhi vigezo vinavyohitajika.**
- (i) **Kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi**
52. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza weledi na ufanisi wa utendaji kazi, Wizara imewevesha watumishi 43 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Kati ya hao watumishi 22 wa kada mbalimbali walihudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi katika ngazi

za Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili, Stashahada ya Uzamili, Shahada na Stashahada. Aidha, Wizara imewezesha watumishi 21 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani za Utunzaji Kumbukumbu, Takwimu Mtandao (e-statistics), TEHAMA, Mfumo wa Manunuvi, Usafirishaji, Utendaji wa Makatibu Mahsusini na Jimolojia.

53. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia ilitoa mafunzo kwa makundi mbalimbali kwa watumishi wa Wizara kama ifuatavyo: watumishi 35 walipatiwa mafunzo ya uandishi na uchambuzi wa Sera; Menejimenti ya Wizara na Maafisa Bajeti wa kila Idara na Kitengo walipatiwa mafunzo ya uandaaji na utengenezaji wa Mkataba wa Utendaji Kazi wa Taasisi; na watumishi 99 walipata mafunzo ya ndani ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) Agosti, 2019.

V. Utekelezaji Katika Maeneo Mengine

(a) Ukaguzi wa Kimkakati

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kudhibiti utoroshaji wa madini nchini kwa kufanya kaguzi maalum na za kimkakati. Kaguzi hizo zimesaidia kubaini wanaotorosha na kufanya biashara haramu ya madini. Katika kipindi rejewa, Wizara ilifanya kaguzi

katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Mwanza, Mara, Arusha, Mbeya na Songwe, ambapo watuhumiwa 95 walikamatwa kati yao 52 tayari wamefikishwa Mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili. Aidha, watuhumiwa 43 waliachiwa baada ya kukosekana ushahidi wa kuwapeleka mahakamani. Kaguzi hizo zilifanywa kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali zikiwemo Kamati za Ulinzi na Usalama katika maeneo husika na Vyombo vya Ulinzi na Usalama.



Picha Na. 8: Baadhi ya Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Watumishi wa Wizara ya Madini Wakishiriki katika Semina ya Udhibiti wa Rasilimali Madini

55. **Mheshimiwa Spika**, kaguzi hizo zimepunguza utoroshwaji wa madini na biashara haramu na hivyo kuongeza utii wa Sheria ya Madini bila shuruti. Hali hiyo ilifanya mauzo ya madini katika masoko na vituo vya ununuzi

kuongezeka. Kwa mfano, katika kipindi cha kuanzia Aprili hadi Novemba 2019, mauzo ya madini ya dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo kuongezeka kutoka gramu 1,188,397.95 hadi gramu 5,546,658.20. Kwa kipindi hicho makusanyo yaliongezeka kutoka **shilingi 7,124,934,647.07** hadi **37,022,685,977.00** sawa na ongezeko la asilimia 420. Aidha, kabla ya kaguzi hizo, idadi ya leseni za biashara ziliwa 696 ikilinganishwa na leseni 1,004 baada ya kaguzi, ikiwa ni ongezeko la leseni 308. Madini yaliyokamatwa yakiuzwa nje ya mfumo rasmi ikiwemo dhahabu, almasi, tanzanite na vito mbalimbali. Madini hayo ambayo yalikuwa na thamani ya jumla ya **shilingi 349,618,546.09** yamehifadhiwa Benki Kuu ya Tanzania wakati taratibu za kisheria zikiendelea.

(b) Ujenzi wa Vituo vya Umahiri, Vituo vya Mfano na Jengo la Taaluma

56. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha ujenzi wa Vituo vinne (4) vya Umahiri ambavyo ni Bariadi, Bukoba, Musoma na Handeni na vimeanza kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Ujenzi wa vituo hivyo umegharimu jumla ya **Shilingi 5,033,286,450.88**. Pia, Wizara ilikamilisha ujenzi wa Jengo la Taaluma la Chuo cha Madini ambalo limegharimu **shilingi**

2,721,110,846.74. Ujenzi wa vituo vitatu (3) vya Umahiri vya Mpanda, Chunya na Songea upo katika hatua za mwisho hadi sasa jumla ya **shilingi 1,661,012,747.06** zimetumika.



Picha Na. 9: Baadhi ya Vituo vya Umahiri kati ya Vituo Saba Vilivyojengwa katika Mikoa Mbalimbali Nchini

57. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Vituo vya Mfano vya Katente – Bukombe na Lwamgasa – Geita umekamilika na viro katika hatua za majaribio. Aidha, Ujenzi wa kituo kingine cha mfano cha Itumbi – Chunya upo katika hatua

za ukamilishwaji. Ujenzi wa vituo vyote vitatu (3) umegharimu jumla ya **shilingi 4,347,098,128.63.**

58. **Mheshimiwa Spika**, vituo hivyo vya mfano ni mahsusini kwa ajili ya kutoa mafunzo mbalimbali kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo. Mafunzo hayo yatahusu uchimbaji na uchenjuaji salama wa madini. Aidha, vituo hivi vitatumika kufanyia maonesho ya madini na vifaa vinavyotumika katika shughuli za uchimbaji madini. Pia wachimbaji wadogo watafundishwa kuhusu uandaaji wa takwimu na taarifa mbalimbali ambazo pamoja na mambo mengine zitakazowasaidia kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha. Vilevile, Wachimbaji Wadogo watapatiwa mafunzo kuhusu tathmini ya mashapo; uongezaji thamani madini; upatikanaji wa taarifa za masoko na utunzaji wa mazingira.

(c) Mnada wa Almasi Shinyanga

59. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya majadiliano na Kampuni ya Petra Diamond Ltd ili iweze kutenga asilimia 5 ya madini yanayozalishwa na kampuni hiyo kwa ajili ya kuuzwa katika soko la ndani. Kampuni ya Petra Diamond Ltd iliridhia jambo hilo. Kwa mara ya kwanza mnada wa almasi ulifanyika nchini tarehe 18 hadi 20 Februari, 2020

katika kituo kidogo cha mauzo ya almasi Mwadui. Lengo la mnada huu ni kuhamasisha biashara ya madini ya almasi nchini.



Picha Na. 10: Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Naibu Waziri wa Madini akishuhudia zoezi la uthaminishaji Madini ya Almasi katika Mnada wa Almasi Mwadui - Shinyanga

60. **Mheshimiwa Spika**, katika mnada huo jumla ya wafanyabiashara wadogo (mineral brokers) 27 walishiriki na kuwasilisha zabuni 122 kwa vifurushi 44 vilivyokuwa sokoni. Kutohana na mnada huo, Serikali ilikusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 39,460,800.29 zilizotokana na mauzo ya shilingi 155,971,542.63 ya almasi kwa vifurushi 11. Fedha hizo zinatokana na malipo ya mrabaha, ushuru wa huduma na ada ya ukaguzi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wadogo wananaufaika na biashara hii ya madini ya almasi na kuimarisha soko la madini Shinyanga.

(d) Uimarishaji wa Taasisi

61. **Mheshimiwa Spika**, Ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Sekta ya Madini, Serikali ilitoa jumla ya **shilingi 10,702,227,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa magari 36, XRF, mizani, kompyuta mpakato na *printer* vitakavyosaidia kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa maduhuli na ununuzi wa vifaa vya masoko. Aidha, Chuo cha Madini (MRI) kilijengewa jengo la taaluma. Ujenzi wa jengo hilo uligharimu **shilingi 2,721,110,846.74**.

(e) Uanzishwaji wa Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited

62. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha majadiliano na kusaini mkataba (Framework Agreement) na kampuni ya Barrick Gold Corporation tarehe 24 Januari, 2020. Mkataba huo, pamoja na mambo mengine umewevesha kuanzishwa kwa kampuni mpya ya *Twiga Minerals Corporation Limited* inayomilikiwa kwa ubia kati ya Serikali (hisa 16%) na Kampuni ya Barrick (hisa 84%). Vilevile, kufuatia kuanzishwa kwa kampuni hiyo Serikali imeshateua wajumbe wa Bodi ikiwa ni hatua ya awali ya kuanza utendaji kazi.



Picha Na. 11 Mhe. Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Tukio la Utiaji Saini wa Mkabata Kati ya Serikali na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Barrick wa kuanzishwa kwa Kampuni ya Ubia ya Twiga Minerals Corporation Limited Januari 24, 2020

63. **Mheshimiwa Spika**, kuanzishwa kwa kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited kutaiwezesha Serikali kuwa mbia mwenza katika miradi ya uchimbaji mkubwa wa madini ili kulinda maslahi mapana ya nchi. Ushirika huu unahusisha migodi yote iliyochini ya Kampuni ya Barrick ambayo ni North Mara Gold Mine Ltd, Bulyanhulu Gold Mine Ltd na Pangea Minerals Ltd (Buzwagi). Hatua hii itaongeza udhibiti zaidi katika shughuli za uzalishaji zinazofanywa na migodi iliyokuwa ikimilikiwa na kampuni ya Barrick Gold Corporation hivyo kuongeza wigo wa mapato kwa Serikali na kufungua milango ya ajira kwa watanzania.

(f) Uzalishaji wa Ajira Katika Sekta ya Madini

64. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Madini imekuwa ikitoa ajira kwa watanzania katika shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020 inakadiriwa kuwa zaidi ya ajira 1,000,505 zilizalishwa ambapo ajira 190,809 ni ajira za moja kwa moja na 809,696 ni ajira zisizo za moja kwa moja.

(g) Masuala Mtambuka

65. ***Mheshimiwa Spika***, katika kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kudhibiti Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) Wizara imeendelea kutoa huduma saidizi kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kwa kutoa fedha taslimu kwa ajili ya huduma ya lishe bora, madawa na vifaa kinga. Aidha, Wizara imekuwa ikiandaa bonanza mbalimbali za michezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha afya za watumishi na ushirikiano mahali pa kazi. Vilevile, wajumbe 20 wa menejimenti ya Wizara pamoja na kamati ya Uadilifu walipatiwa mafunzo Machi, 2020 kuhusu masuala ya rushwa na athari zake.

66. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuunga mkono juhudini mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID – 19) kwa kuhakikisha watumishi na wadau wa Sekta ya Madini wanafuata na kuzingatia ushauri wa kitaalam unaotolewa na Serikali.

(h) Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Baruti

67. ***Mheshimiwa Spika***, Matumizi ya baruti ni muhimu sana katika shughuli za uchimbaji madini na ujenzi wa miundombini mbalimbali. Hata hivyo, matumizi ya baruti yasiyozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu yanaweza kusababisha athari kubwa za kiusalama, kiafya na uharibifu wa mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Wizara iliendelea kusimamia na kudhibiti matumizi ya baruti kwa kuhakikisha kuwa watumiaji wa baruti wanaingiza, wanasafirisha, wanatunza na kutumia baruti kwa kufuata Sheria ya Baruti Sura ya 45 na Kanuni zake. Wizara imefanya kaguzi katika maghala 26 ya kuhifadhia baruti katika maeneo ya Lugoba-Pwani, Kilosa-Morogoro, Geita, Ihumwa-Dodoma, Mirerani-Manyara, Rufiji - Pwani na Nzega-Tabora. Ukaguzi huo ulihusu taratibu za ununuzi, usafirishaji, matumizi, utunzaji

wa kumbukumbu za baruti na utunzaji wa mazingira kuzunguka maghala ya baruti.

68. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi rejewa, jumla ya vibali 170 vya kuingiza baruti nchini vilitolewa na leseni 28 za maghala ya kuhifadhia baruti katika maeneo ya Dodoma, Rufiji, Geita, Nzega, Musoma, Mirerani na Mbozi zilitolewa na kibali cha kujenga maghala Buhalahala – Geita kilitolewa. Aidha, jumla ya tani 22,233 za baruti zimetumika migodini na vipande 2,745,018 vya fataki viliingizwa nchini kwa shughuli za ulipuaji kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini na ujenzi wa miundombinu mbalimbali.
69. **Mheshimiwa Spika**, ukaguzi ulifanyika pia katika kiwanda cha kutengeneza baruti cha kampuni ya *Nitro Explosive Ltd* kilichopo Kilwa-Lindi. Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kujiridhisha na utekelezaji wa Sheria ya Baruti Sura ya 45 na Kanuni zake kwa kampuni hiyo kwa lengo la kutoa kibali cha kutengeneza Baruti. Aidha, ukaguzi wa matumizi ya baruti ulifanyika katika eneo la Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere Hydropower ulioko Bonde la Mto Rufiji kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya baruti.
70. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na wamiliki wengi wa maghala ya baruti kutekeleza wajibu

wao, kaguzi zilibaini uwepo wa baadhi ya wamiliki wa maghala kutotunza ipasavyo mazingira kuzunguka maghala yao. Aidha, katika mradi wa ujenzi wa reli ya kati ya kisasa kwa kiwango cha Kimataifa – *Standard Gauge Railway* (SGR) kulikuwa na changamoto ya kutokadiria vizuri matumizi ya baruti kwenda kwenye maeneo ya kazi hivyo kusababisha baruti nyingi kurudi ghalani. Kufuatia changamoto zilizobainika, Wizara iliwataka wadau husika kurekebisha mapungufu hayo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya taratibu za ununuza, usafirishaji, matumizi, utunzaji wa kumbukumbu za baruti na utunzaji wa mazingira kuzunguka maghala ya baruti. **Hivyo, napenda kuwasihhi wadau wa baruti kufanya shughuli zao kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia baruti.**

(i) Uelimishaji Umma kuhusu Sekta ya Madini Nchini

71. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilianzisha kampeni ya kuelimisha Umma iliyopewa jina la '**Madini Yatatutoa**'. Kampeni hiyo ililenga kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sekta ya Madini, kutambua fursa zilizopo na kuzitumia. Aidha, kampeni hiyo ilielezea mafanikio yaliyopatikana kwenye Sekta ya Madini kufuatia Marekebisho ya Sheria ya Madini

Sura ya 123. Kampeni iliendeshwa kupitia vipindi mbalimbali vya Redio, Runinga na pia kusambazwa katika Tovuti ya Wizara na mitandao mbalimbali ya kijamii.



Picha Na. 12: Mh. Stanslaus Nyongo Naibu Waziri wa Madini (Kushoto) na Katibu Mkuu wa Madini Prof. Simon Msanjila (kulia) kwa nyakati tofauti wakishiriki katika Kipindi cha Jambo Tanzania (TBC1) ikiwa ni sehemu ya kampeni ya kuelimisha Umma ya ‘Madini Yatatutoa’

72. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Habari - MAELEZO, iliandaa Kipindi Maalum kuonesha Mafanikio ya Uanzishwaji wa Soko la Madini la Chunya na mchango wake katika kukuza uchumi wa eneo hilo. Taarifa kuhusu kipindi hicho zilisambazwa katika mitandao ya kijamii, Magazeti na Vyombo vingine vya habari.
73. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia iliratibu ushiriki wa Viongozi Wakuu na Waandamizi

wa Wizara katika Vipindi Maalum vya Redio na Runinga. Lengo la vipindi hivyo lilikuwa ni kuelimisha na kutoa ufanuzi kwa Umma kuhusu masuala mbalimbali yanayoishus Sekta ya madini. Masuala hayo ni pamoja na: Sheria ya Madini Sura ya 123, wajibu wa wamiliki wa leseni za uchimbaji madini kwa jamii zinazoizunguka migodi (CSR), ushiriki wa nchi na wananchi katika mnyororo wa uchumi wa madini (Local Content). Aidha, elimu kuhusu aina mbalimbali za leseni za madini, matumizi na faida ya Masoko na Vituo vya kuuzia na kununua madini (Buying Centres) na uwekezaji katika Sekta ya Madini ilitolewa.

**(j) Uundwaji wa Mfumo wa Kufuatilia
Mwenendo wa Masoko ya Madini**

74. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanikisha kuundwa kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Masoko ya Madini wa kufuatilia mwenendo wa mauzo. Mafunzo ya matumizi ya mfumo huo yamefanyika kwa wafanyakazi wa masoko ya madini yaliyopo katika Mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Lindi, Njombe, Mtwara, Manyara, Songwe, Ruvuma, Kagera na Shinyanga. Mfumo huu ulianza kutumika Januari, 2020. Aidha, mafunzo hayo yanaendelea katika mikoa mingine iliyobaki. Miiongoni mwa taarifa zinazopatikana mubashara kuitia mfumo huo

ni kiasi cha madini yaliyofika sokoni, mauzo, bei na maduhuli ya Serikali yaliyokusanywa kupitia mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Mfumo huo unasaidia katika upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati za mauzo. Mfumo huo umebuniwa na kutengenezwa na wataalam wetu wa ndani hivyo kuepuka gharama zisizo za lazima kwa kutumia wataalam kutoka nje. Mfumo huo unapatikana kupitia kikoa kidogo cha <https://masoko.madini.go.tz>.

(k) Kuimarisha Ulinzi Eneo Tengefu la Mirerani

75. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Pamoja (One Stop Centre) ndani ya ukuta wa Mirerani. Aidha, ufungaji wa miundombinu ya umeme na taa umekamilika na ufungaji wa kamera za ulinzi (CCTV) kuzunguka eneo la ukuta wa migodi ya madini ya tanzanite upo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa, shughuli zote zinazohusu biashara ya madini ya tanzanite zinafanyika ndani ya ukuta. Hatua hii itaimarisha upatikanaji wa takwimu, kudhibiti utoroshaji wa madini ya tanzanite na kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.



Picha Na. 13: Muonekano wa Mfumo wa Ulinzi wa CCTV kamera, Jengo la Kituo cha Pamoja na Ukuta Kuzunguka machimbo ya Tanzanite Mirerani – Manyara

76. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa ukuta umesababisha kuongezeka kwa makusanyo ya Serikali kwa takribani mara 13 ya kiwango kilichokuwa kikikusanya awali. Kwa mfano, katika mwaka 2019 makusanyo yaliongezeka na kufikia **shilingi 2,150,000,000** ikilinganishwa na **shilingi 166,094,043**

zilizokusanywa mwaka 2017 kabla ya ujenzi wa ukuta.

(1) Shughuli za Kiutawala na Kiutumishi

77. **Mheshimiwa Spika**, Wizara na Taasisi zake imepokea jumla ya watumishi 220 kwa utaratibu wa ajira mpya, ajira mbadala na uhamisho kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali. Kati ya hao, watumishi 16 walijiriwa Wizarani, 188 Tume ya Madini, wanne (4) STAMICO, wanane (8) GST, wawili (2) Chuo cha Madini (MRI) na wawili (2) Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC). Kupatikana kwa watumishi hao kumepunguza changamoto ya upungufu wa watumishi hivyo, kusaidia Wizara na Taasisi zake katika utekelezaji wa majukumu yake.

KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA MADINI

78. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Madini inasimamia taasisi sita (6) ambazo ni: Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI); Chuo cha Madini (MRI); na Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC).

i. Tume ya Madini

79. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Madini iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura ya 123, ikiwa na majukumu mbalimbali ikiwemo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kuimarisha ukaguzi wa masuala ya usalama, afya, mazingira, uzalishaji na biashara ya madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kudhibiti utoroshaji wa madini; na kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini.

(a) Uzalishaji na Ukusanyaji wa Maduhuli

80. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi kinachoanzia mwezi Julai, 2019 hadi Februari, 2020 jumla ya kilo 25,435.12 za dhahabu zenye thamani ya **shilingi 2,772,331,030,317.99** zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka katika Migodi Mikubwa na ya Kati. Migodi hiyo ni pamoja na Geita Gold Mine, North Mara Gold Mine, Pangea Minerals (Buzwagi Mine), Bulyanhulu Gold Mine, Shanta Mine (New Luika), STAMIGOLD Company (Biharamulo Mine) na Busolwa Gold Mine (Tanzania). Aidha, katika

kipindi hicho kilo 10,102.43 za dhahabu zenyе thamani ya **Shilingi 975,430,320,903.97** zilizalishwa na wachimbaji wadogo wa madini.

81. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi tajwa kiasi cha **karati 201,547.71** za madini ya almasi yenе thamani ya **shilingi 84,377,839,160.40** yalizalishwa katika Mgodi wa almasi wa Mwadui (Williamson Diamond Limited), na **karati 8,680.05** zenyе thamani ya **shilingi 5,472,619,953.21** zilizalishwa na wachimbaji wadogo wa almasi. Aidha, wachimbaji wadogo wa madini ya tanzanite wamezalisha tanzanite ghafi kiasi cha **kilogramu 3,798.70**; tanzanite zilizokatwa na kusanifiwa ni kiasi cha **karati 95,104.50**; kiasi cha **kilogramu 26,343.86** ni cha madini ya tanzanite yenе ubora wa chini (Beads); na madini mengine ya vito kiasi cha **tani 1,120** kilizalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.
82. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa makaa ya mawe, jumla ya **tani 430,761.32** zilizalishwa kwenye Mgodi wa Ngaka na Kambas Mining Investment Mkoa wa Ruvuma; **tani 9,908.43** katika Mgodi wa Kabulo – Songwe; na **tani 2,733.19** katika Mgodi wa Edenville – Sumbawanga-Rukwa.

Aidha, **tani 22,036,068.64** za madini ya ujenzi na **tani 951,906.57** za madini mengine ya viwandani zilizalishwa katika maeneo mbalimbali nchini. Pia, **tani 7,046** za madini ya kinywe (Graphite) zilizalishwa kutoka katika Mgodi wa GodMwanga Mirerani.

83. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na uzalishaji wa madini mbalimbali nchini, hadi kufikia Machi, 2020 Tume ya Madini ilikusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 358,643,870,797** sawa na **asilimia 102** ya lengo la **shilingi 352,765,797,750** kwa kipindi hicho. Makusanyo hayo yalitokana na malipo ya mrabaha, ada ya ukaguzi, ada ya pango ya mwaka, ada za kijiolojia, faini mbalimbali na mapato mengineyo.

(b) Utoaji wa Leseni

84. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Tume ya Madini ilitoa jumla ya **Leseni 5,935** za madini kwa mchanganuo ufuatao: Leseni 13 za Uchimbaji wa Kati wa Madini (MLs); Leseni 102 za Utafutaji wa Madini (PLs); Leseni 2,801 za Uchimbaji Mdogo (PMLs); Leseni kubwa 601 za biashara (DL); Leseni ndogo 2,376 za biashara (BL); Leseni 38 za Uchenjuaji wa Madini (PCLs); Leseni 2 za Usafishaji wa

Madini (RFL); na Leseni 2 za uyeyushaji Madini (SL).

85. **Mheshimiwa Spika**, kati ya leseni zilizotolewa, **asilimia 47.20** ni za wachimbaji wadogo. Hii inadhihirisha kuwa Serikali ya Awamu ya Tano, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa kipaumbele kwa Watanzania kushiriki ipasavyo katika Sekta ya Madini ili wanufaikie na rasilimali hizi ambazo tumejaliwa na Mwenyezi Mungu.

(c) Ukusanyaji wa Maduhuli kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali (GePG)

86. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelekezwa na Serikali, Tume ya Madini iliendelea kutumia mfumo wa GePG katika Ukusanyaji wa Maduhuli. Kupitia mfumo huo, Tume ina uwezo wa kupata taarifa za makusanyo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mrabaha na tozo mbalimbali za madini kwa wakati. Mfumo huo pia umeondoa changamoto zilizokuwa zikiambatana na matumizi ya risiti za ERVs zikiwamo upatikanaji kwa wakati kwa vitabu hivyo na muda unaotumiwa na wateja kulipa na kufuatilia risiti hizo.

(d) Ukaguzi wa Migodi

87. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Madini iliendelea na utekelezaji wa jukumu la ukaguzi wa migodi ambalo ni muhimu katika Sekta ya Madini. Lengo la kaguzi hizo ni kuangalia jinsi migodi inavyotekeleza Sheria na Kanuni mbalimbali za Madini na Mazingira. Kaguzi zilifanyika katika Migodi ya wachimbaji wakubwa, wa kati na wadogo. Kaguzi hizo zilihusisha migodi ya wachimbaji wakubwa ikiwemo Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi; Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu; Mgodi wa Dhahabu wa North Mara; Mgodi wa Dhahabu wa Geita na Mgodi wa almasi wa Mwadui (WDL).



Picha Na. 14: Timu ya Wakaguzi ikiwa katika Ukaguzi wa Mgodi

88. **Mheshimiwa Spika**, ukaguzi huo pia ulifanyika katika migodi ya wachimbaji wa kati ikiwemo ya Nsoromero Minerals Co-operative Society Ltd; Mara Mine Development Ltd; Nyamongo (T) Ltd; Nyamongo Gold Mine Ltd; P.Z. Gold Mining Co. Ltd; MMG Gold Ltd; CATA Mining Co. Ltd; Perfallbion Minerals Ltd; ZEM (T) Co. Ltd; Sunshine Ltd; na Zem Development Co. LTD.
89. **Mheshimiwa Spika**, kaguzi hizi zilifanyika pia kwenye migodi zaidi ya 100 ya wachimbaji wadogo katika maeneo yenye shughuli za uchimbaji madini nchini. Ukaguzi huo ulifanyika katika mikoa ya Manyara, Geita, Kagera, Shinyanga, Singida na Tabora.
90. **Mheshimiwa Spika**, matokeo ya kaguzi hizi yalibaini kufanyiwa kazi kwa mapungufu yaliyoonekana katika kaguzi zilizotangulia. Hata hivyo, kaguzi zilibaini kuendelea kuwepo kwa mapungufu kadhaa ikiwemo uendeshaji wa shughuli za madini usiozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu hususan zinazohusiana na utunzaji wa mazingira. Migodi ilielekezwa kufanya marekebisho katika mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kaguzi hizo.


ii. Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

91. **Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa la Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ni kufanya tafiti za jiosayansi na ugani wa jiolojia kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia tafiti hizi taarifa mbalimbali za jiosayansi za uwepo wa madini nchini zinaandaliwa ili kuhamasisha uwekezaji katika utafiti wa kina (detailed exploration) kwa lengo la kuanzisha migodi mipya. Aidha, taarifa hizi za jiosayansi zinatumika katika sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, maji, ujenzi, na mipango miji. Vilevile, GST ina jukumu la kuratibu majanga ya asili ya jiolojia kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, kemikali hatarishi pamoja na maporomoko ya udongo.

(a) Ugani/Utafiti wa Jiosayansi na Uboreshaji Ramani za Jiolojia na Upatikanaji wa Madini

92. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, GST iliendelea kufanya ugani/utafiti wa jiosayansi na kuboresha ramani za jiolojia na taarifa za upatikanaji wa madini. Katika utafiti huo, GST ilikamilisha ugani wa jiolojia na jiokemia katika QDS 293

iliyohusisha Kata za Kibutuka, Chiola, Kipara Mnero, Lionja, Marambo, Mkoka, Mkotokuyana, Mnero, Mnero-ngongo, Mpiruka, Mtua, Naipingo, Namapwia, Namatula, Nambambo, Namikango, Nangowe, Nditi, Ruponda, Chienjere, Likunja, Luchelegwa, Makanjiro, Mandarawe, Mbekenyera, Mnacho, Narungombe, Nkowe, katika wilaya ya Nachingwea na Ruangwa mkoa wa Lindi. Ramani pamoja na maelezo yake zipo katika hatua ya kuhaririwa kwa ajili ya uchapishwaji. Matokeo ya awali ya utafiti huo yalionesha kuwa katika QDS 293 kuna madini ya kinywe (graphite) yenye ubora mkubwa (flake graphite) na viashiria vyatuhabu.



Picha Na. 15: Wajiolojia wakichunguza na kukusanya takwimu kuhusu miamba katika eneo la QDS 293 lililopo Nachingwea mkoani Lindi

93. **Mheshimiwa Spika**, GST ilikamilisha uhakiki (field checks) wa ramani za jiolojia katika QDS tano (5) ambazo ni 267 na 268 zilizopo Mkoa wa Lindi, 160, 121, na 122 zilizopo Mkoa wa Singida. Ramani pamoja na maelezo yake (explanatory notes) kwa QDS 267, 268 na 160 zimekamilika na kuchapishwa. Ramani za QDS 121 na 122 zipo katika hatua za kuhaririwa (editing) ili ziweze kuchapishwa. QDS 121 na 122 zina viashiria vya uwepo wa madini ya dhahabu na shaba. Uchunguzi wa sampuli katika maeneo mengine bado unaendelea.
94. **Mheshimiwa Spika**, GST kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilikamilisha utafiti wa jiolojia na uchoraji wa ramani katika QDS nne (4) ambazo ni QDS 38, 39, 52 na 53 zenyenye jumla ya kilomita za mraba 11,664. Ramani maalum inayoonesha maeneo mapya ya utalii wa jiolojia (geosites) ilichorwa na taarifa ya maelezo ya kina ya geosite hizo imeandaliwa. Vivutio hivyo ni *Embulmbul depression* lililosababishwa na bonde kuu la ufa la Afrika Mashariki; *Moving Sand* - mchanga ambao unasadikiwa kwamba huwa unatembea; *Engaresero gorge* – eneo lenye maporomoko ya maji ambalo limekuwa kivutio kikubwa cha watalii; *Nasera rock* - jiwe kubwa la kuvutia lililotokana na kupanda kwa magma iliyobeba mchanganyiko wa

chembechembe za madini na kisha ukapoa na kutengeneza jabali kubwa la mwamba juu ya uso wa ardhi.

(b) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za Jiosayansi

95. ***Mheshimiwa Spika***, GST imefanya tafiti za jiolojia na kutoa mrejesho wa tafiti hizo kwa wachimbaji wadogo. Baada ya kukamilika kwa tafiti hizo mafunzo juu ya namna bora ya kutambua miamba yenyenye mashapo na kuchenjua madini yalitolewa kwa wachimbaji wadogo 180. Mafunzo hayo yalitolewa katika maeneo ya Muhintiri na Mang'onyi mkoa wa Singida pamoja na Musasa na Matabe Wilaya ya Chato. Maeneo mengine ni Foresti Wilaya ya Bukombe na Mgusu Wilaya ya Geita. Lengo la tafiti hizo ilikuwa kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata taarifa sahihi kuhusu mashapo. Taarifa hizo zitasaidia kuongeza uzalishaji na hatimaye kuongeza kipato na kuboresha maisha ya wachimbaji wadogo.
96. ***Mheshimiwa Spika***, utafiti mwingine ulifanyika katika eneo la wachimbaji wadogo Nholi Mkoa wa Dodoma ili kubaini namna bora ya kuchenjua madini ya dhahabu kutoka kwenye mbale. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa: mbale iliyopo maeneo ya Nholi ina dhahabu kiasi cha wastani wa

gramu 1.98 kwa kila tani moja ya mbale; wachimbaji wadogo wanapata dhahabu kutoka kwenye mbale kwa kiwango cha **asilimia 70** tu baada ya kuchenjua kwa kutumia zebaki. Utafiti ulifanywa kwa njia ya kuozesha sampuli kwa kutumia sayanaidi na matokeo yake yalionesha kuwa, upatikanaji wa dhahabu kutoka katika mbale uliongezeka kutoka **asilimia 70** hadi **87**. Hata hivyo, utafiti unaendelea ili kubaini njia bora zaidi ya kuchenjua dhahabu ili kuongeza uzalishaji na tija kwa wachimbaji wadogo. **Nitoe rai kwa wachimbaji wadogo kuitumia Taasisi ya GST katika kutambua tabia za mbale za eneo husika ili kuweza kutumia njia sahihi ya uchenjuaji kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji.**

(c) Tafiti Maalum za Jiosayansi

97. **Mheshimiwa Spika**, tafiti maalum za jiosayansi ni tafiti ambazo zinafanywa kutatua changamoto zilizojitekeza katika maeneo mbalimbali ya nchi. Mfano kwenye maeneo mapya yaliyogundulika/kusadikika kuwa na madini na kuvamiwa na Wachimbaji (mineral rush); kuhitaji taarifa zaidi za jiosayansi kwenye eneo maalum; na maagizo au maombi kutoka kwa viongozi mbalimbali pamoja na wananchi kwa ujumla.

98. **Mheshimiwa Spika**, GST ilifanya tafiti katika eneo la Mradi wa Ufuaji Umeme wa Bonde la Rufiji (Julius Nyerere Hydropower Project) kwa lengo la kubaini uwezekano wa uwepo wa Makaa ya Mawe. Uchunguzi ulifanyika katika maeneo ya uchorongaji na uandaaji wa mifereji ya uchepushaji wa maji ikiwa ni pamoja na sehemu ya *inlet tunnel, outlet tunnel, adit* pamoja na kukusanya taarifa za jiolojia za sampuli za miamba choronge (rock cores). Uchunguzi huo ulithibitisha kutokuwepo kwa makaa ya mawe katika eneo lililofanyiwa utafiti. Wizara itaendelea kupeleka wataalam katika maeneo ya miradi mbalimbali inayohusisha uchorongaji wa miamba ili kuweza kubaini uwepo wa madini katika maeneo hayo.
99. **Mheshimiwa Spika**, Utafiti wa pili ulifanyika na kukamilika katika eneo la Lukwika wilaya ya Nanyumbu na kubaini uwepo wa madini ya dhahabu. Aidha, utafiti mwingine ulifanyika katika eneo la Kisisi Godegode na maeneo mengine katika Wilaya za Mpwapwa na Kilosa ambako ujenzi wa SGR unafanyika ili kubaini uwepo wa madini. Uchunguzi ulikamilika na kubaini kuwepo kwa miamba iliyobeba madini ya *ruby-corundum* na *red garnet* ambapo madini hayo hayakuwa na ubora wa kukidhi kuwa vito vya thamani. Pia, ili kuhakikisha Serikali inapata taarifa sahihi kuhusu uwepo

ama kutokuwepo kwa rasilimali madini katika maeneo mbalimbali ya mradi wa SGR. Wizara imepeleka mtaalamu wa jiosayansi ambaye atakuwa anakusanya taarifa za jiolojia ili kubaini kama kuna madini ya thamani kubwa katika eneo la mradi husika.



Picha Na. 16. Katibu Mkuu Wizara ya Madini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilano (Uchukuzi) wakiwa katika ziara ya kukagua uwepo wa madini katika eneo la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

(d) Kuboresha huduma za Maabara kwa wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi

100. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa GST inaendelea kutoa huduma za maabara zinazokidhi viwango vyta kimataifa, maboresho ya mifumo ya uendeshaji

yalifanyika. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kupitia ukaguzi uliofanywa na taasisi ya SADCAS inayosimamia ubora wa huduma za maabara katika Ukanda wa SADC, maabara ya GST ilikidhi vigezo vyta kimataifa katika uchunguzi wa madini ya dhahabu. Hatua hii iliwezesha GST kupata ITHIBATI ya kimataifa ya uchunguzi wa sampuli za dhahabu kwa njia ya tanuru (fire assay) na kupewa **ISO: 17025** tarehe 15 Oktoba, 2019.



Picha Na. 17: Wataalam wa Maabara ya GST Wakifanya Uchunguzi wa Sampuli

101. **Mheshimiwa Spika**, jukumu lingine la GST ni kufanya uchunguzi wa sampuli za wateja na ambazo zinahitaji vibali kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya sampuli 6,167 zilifanyiwa uchunguzi. Kati ya hizo, sampuli 5,596 zilikuwa za wateja na sampuli 572 kwa ajili ya kupata vibali vyta kusafirisha kwenda nje ya nchi. Aidha, jumla ya vyungu vikubwa vyta kuyeyushia sampuli za

dhahabu (crucibles) 2,869 na vyungu vidogo (Cupels) 2,011 vilizalishwa.



Picha Na. 18: Vyungu vya kuyeyushia dhahabu (crucibles) na Cupels mara baada ya kutengenezwa katika maabara ya GST

(e) Kuboreshwa kwa Kanzidata ya Jiosayansi

102. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hili, kampuni nane (8) zinazojihusisha na shughuli za madini kutoka Mikoa ya Mtwara na Lindi zilitembelewa kwa ajili ya kukusanya taarifa, kukagua mawe choronge (cores) zilizopo pamoja na kuzikumbusha wajibu na utaratibu wa kisheria wa uwasilishwaji wa taarifa/takwimu GST. Aidha, GST ilishiriki mashindano ya uchakataji wa picha za satelaiti (remote sensing data processing) yaliyofanyika nchini Botswana. Mashindano hayo yalilenga kuainisha maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuwa na madini

kwa ufuatiliaji zaidi. Mashindano hayo yaliyohusisha nchi 12 za SADC. Katika mashindano hayo, GST ilishika nafasi ya nne na mwakilishi wake aliweza kutunukiwa cheti cha kuwa mkufunzi kwa nchi za Kusini mwa Afrika na kufanya idadi ya wakufunzi kutoka Tanzania kufikia wanne (4). Hii imeendelea kudhihirisha umahiri wa wataalam wetu wa ndani katika masuala ya uchakataji wa takwimu na taarifa za jiosayansi.

(f) Kukabiliana na Majanga ya Asili ya Jiologya

103. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na majanga ya asili ya jiologya na kutoa ushauri wa namna bora ya kupunguza madhara yanayoweza kutokana na majanga hayo, GST ilikusanya takwimu za matetemeko ya ardhi kutoka katika vituo vya kuratibu matetemeko ya ardhi vya Mtwara, Arusha, Mbeya, Geita na Dodoma. Takwimu zilichakatwa na kubaini kuwepo kwa matetemeko ya ardhi yaliyotokea kwa nyakati tofauti katika maeneo ya Kijiji cha Ngulu Mkoa wa Tabora, Nala na Haneti Mkoa wa Dodoma, Naberera Mkoa wa Manyara na Kijiji cha Sibwesa Mkoa wa Katavi. Matetemeko hayo yalikuwa na ukubwa wa kati ya 2.7 na 5.5 katika kipimo cha Richter. Taarifa za matetemeko hayo ya ardhi ziliandaliwa na kusambazwa kwa mamlaka

husika na vyombo vy a habari kwa lengo la kutoa tahadhari na kuelimisha jamii.

104. **Mheshimiwa Spika**, GST ilikamilisha uchunguzi kuhusu tukio lililosadikiwa kuwa ni volkano katika Kata ya Ndembesi Manispaa ya Mji wa Shinyanga. Uchunguzi ulibaini kwamba kulikuwa na tabaka la tope lililochanganyika na maji ambalo lilibubujika na kusukumwa kuja juu ya uso wa ardhi. Tukio hilo kitaalam huitwa *Liquefaction* na siyo volkano. Baada ya uchunguzi huo GST ilitoa taarifa kwa uongozi wa eneo husika ikiwa ni pamoja na uongozi wa Wilaya na Mkoa wa Shinyanga na kwa wananchi kwa ujumla kupitia vyombo vy a habari kwa lengo la kuwatoa wasiwasi juu ya tukio hilo.
105. **Mheshimiwa Spika**, GST ilikamilisha uchunguzi kuhusu tukio lililotokea tarehe 11 Desemba, 2019 la kusadikiwa kuwepo kwa tukio la volkano katika kitongoji cha Sang'ombe Kijiji cha Tatwe, Kata ya Gulibe Wilayani Rarya katika Mkoa wa Mara. Matokeo ya uchunguzi yalibaini kuwa tukio hilo lilikuwa ni maporomoko ya ardhi (landslide) yaliyosababishwa na kuwepo kwa mvua nyingi. GST ilitoa taarifa ya tukio hilo kwa wananchi wa kijiji cha Tatwe na kwa uongozi wa Wilaya na Mkoa wa Mara na kwa Taifa kwa ujumla kupitia vyombo vy a habari.

iii. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

106. **Mheshimiwa Spika**, majukumu makuu ya STAMICO baada ya maboresho ya hati ya uanzishwaji wake kuitia Gazeti la Serikali (GN) 171 ya mwaka 2015 ni pamoja na: kuwekeza kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji, na uchenjuaji wa madini; kutoa huduma za kibiashara za uchorongaji miamba; utafutaji wa madini; kutoa ushauri elekezi wa masuala ya mazingira pamoja na kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini kwa kutoa ushauri wa kitaalam kwa wachimbaji hao.
107. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Shirika lilikukusanya kiasi cha **shilingi 4,125,871,300.34** sawa na **asilimia 113** ya lengo la makusanyo ya **shilingi 3,663,954,619.00** katika kipindi husika. Makusanyo hayo yalitokana na vyanzo vya ndani vya Shirika.
- (a) **Uwekezaji katika Shughuli za Utafutaji, Uchimbaji, Uchenjuaji wa Madini**
108. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa shughuli za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini nchini, mionganii mwa miradi iliyotekelizwa na Shirika ni kama ifuatavyo:

Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kabulo/Kiwira

109. **Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea na uchimbaji wa makaa ya mawe katika kilima cha Kabulo kilichopo eneo la Kiwira, Mkoani Songwe. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Shirika lilizalisha jumla ya tani 9,908.43 za makaa ya mawe ambapo kati ya hizo tani 4,419.10 ziliuzwa. Kutokana na mauzo hayo Shirika lilipata kiasi cha **shilingi 271,642,828.65** na kulipa serikalini kiasi cha **shilingi 30,825,217.98** kama mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Aidha, ili kuongeza mapato, STAMICO imeingia Mkataba na Mbeya Cement Company Ltd ili kuwauzia makaa ya mawe. Kadhalika, Shirika lipo kwenye hatua za mwisho za makubaliano na kiwanda cha Sunflag Tanzania Ltd kilichopo Arusha ili kuweza kuwauzia makaa ya mawe.

Mgodi wa Dhahabu wa STAMIGOLD

110. **Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya STAMIGOLD ambayo ni kampuni Tanzu ya STAMICO kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Februari, 2020 imeweza kuzalisha na kuuza wakia 9107.45 za madini ya dhahabu na wakia 1,170.21 za madini ya fedha, vyote vikiwa na thamani ya **shilingi**

31,539,991,237.11. Mgodi umelipa jumla ya **shilingi 2,303,564,360.31** kwa ajili ya malipo ya mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Aidha, mgodi umeanza kuuza dhahabu inayozalisha kwenye masoko ya ndani ya madini. Hatua hii imeokoa gharama ya usafirishaji kiasi cha **shilingi milioni 131.8** kama dhahabu ingeuzwa nje ya nchi.



Picha Na. 19: Mtambo wa kuchenjua dhahabu katika Mgodi wa STAMIGOLD

Mradi wa kusafisha dhahabu wa Mwanza

111. **Mheshimiwa spika**, Shirika limeanza ujenzi wa mradi wa kusafisha dhahabu (gold refinery) jijini Mwanza. Mradi huo wa ubia unatarajiwa

kukamilika Desemba, 2020 na kwa kuanzia utakuwa na uwezo wa kusafisha dhahabu wastani wa **kilo 480** kwa siku. Mradi huu utagharimu jumla ya **Dola za Marekani milioni 58.204**. Kwa sasa kampuni ya ubia imeashaanzishwa kwa jina la *Mwanza Precious Metals Refinery*. Ujenzi wa mtambo huu wa kusafisha dhahabu wenyе teknolojia ya kisasa utasafisha dhahabu mpaka kufikia kiwango cha **999.9 purity** unatarajiwa utaongeza mapato ya nchi kupitia mrabaha na tozo mbalimbali pamoja na kuongeza ubora wa dhahabu ya Tanzania kimataifa.



Picha Na. 20: Mchoro Wa Kitakachokuwa Kiwanda Cha Kusafisha Dhahabu Jijini Mwanza

Mradi wa Dhahabu wa Buhemba

112. **Mheshimiwa spika**, Shirika pia limeanza utekelezaji wa mradi wa kuchimba dhahabu

wa Buhemba ambao makadirio ya gharama za awali za mradi huo ni **Dola za Marekani milioni 24**. Kwa sasa taratibu za kuagiza mtambo wa kuchenjua dhahabu zinaendelea baada ya majibu ya sampuli kupatikana kutoka katika maabara za nje na ndani ya nchi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Desemba, 2020.


(b) Uendelezaji wa Leseni za Shirika

113. **Mheshimiwa Spika** Shirika limeendelea kufanya utafiti wa leseni zake ili liweze kuziendeleza. Aidha, katika kipindi rejewa, Shirika pia limeweza kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Kampuni ya Madini ya kutoka nchi ya Indonesia PT TIMAH ili kuendeleza leseni za Shirika. Katika kuanza kutekeleza makubaliano hayo timu ya wataalamu wa Kampuni ya PT TIMAH pamoja na wataalamu wa Shirika wameshapitia maeneo ya leseni za Shirika ili kuainisha leseni za kuanza kuziendeleza.

(c) Huduma za Uchorongaji

114. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Shirika limeendelea kutoa huduma za kibashara za uchorongaji miamba katika Sekta ya Madini na Mafuta. Shirika limefanikiwa kupata kandarasi nne za

uchorongaji. Kati ya hizo, kandarasi 3 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.99 zimekamilika. Aidha, katika jitihada za kuimarisha shughuli za uchorongaji Shirika limeweza kutangaza shughuli zake za uchorongaji katika makampuni mbalimbali ya madini nchini. Kwa sasa Shirika lipo katika mazungumzo na Migodi mikubwa na ya kati kwa lengo la kupata kandarasi za uchorongaji. Napenda kutoa rai hususan kwa wachimbaji wadogo kutosita kuwasiliana na STAMICO pale wanapohitaji huduma hiyo.



Picha Na. 21: Wataalam wa STAMICO wakiwa katika Shughuli za Uchorongaji

115. **Mheshimiwa spika**, kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho, Shirika

linatarajia kuchangia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kiasi cha shilingi bilioni 1.1 katika mfuko wa Serikali. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa huu ni mwanzo tu, kutokana na maboresho yanayoendelea ya kimuundo pamoja na usimamizi wa karibu wa Shirika, tija zaidi itaendelea kuonekana.

(d) Huduma kwa Wachimbaji wadogo

116. **Mheshimiwa Spika,** Shirika linaendelea kuratibu shughuli za uchimbaji mdogo nchini. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/2020 Shirika limekamilisha usimamizi wa ujenzi wa Vituo vya Mfano kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya Katente na Lwamgasa ambavyo kwa sasa viro katika uzalishaji wa majaribio. Aidha, Kituo cha Itumbi kipo katika hatua za mwisho za kukamilishwa. Vituo hivyo vitatoa mafunzo ya vitendo katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo.
117. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limewezesha vikundi vitano (5) vya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Singida, Kilindi na Morogoro kuelewa jiolojia ya maeneo yao ili kuweza kuainisha maeneo ya kuchimba na kupanga namna bora ya uchimbaji katika maeneo hayo. Vilevile, Shirika lilishirikiana na Chama cha Wachimba Madini Mkoa wa Geita, na Mpango

wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo zaidi ya 950 kuhusu upatikanaji wa leseni za uchimbaji mdogo, uchimbaji salama na uchenjuaji yaliyofanyika katika wilaya zote za Mkoa wa Geita.

iv. Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

118. ***Mheshimiwa Spika***, moja ya majukumu ya TEITI ni kuimarisha na kuboresha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, Desemba, 2019 TEITI iliweka wazi kwa umma Ripoti ya Ulinganishi wa Malipo ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na Mapato ya Serikali kwa Mwaka 2016/2017. Ripoti hiyo imeonesha kuwa Serikali ilipokea **shilingi 441,831,277,513.46** kutoka katika Kampuni 22 za Madini, Mafuta na Gesi Asilia zilizoingia katika zoezi la ulinganishi. Aidha, TEITI inatarajia kukamilisha ripoti ya ulinganishi wa malipo ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na Mapato ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 kabla ya Julai, 2020.
119. ***Mheshimiwa Spika***, ripoti ya nane (8) ya TEITI ya mwaka 2015/2016 ilionesha tofauti ya **shilingi bilioni 30** kati ya mapato na

malipo yaliyopokelewa kutoka Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia zilizofanyiwa ulinganishi. Kwa mujibu wa Sheria ya TEITA ya Mwaka 2015 ripoti hiyo inatakiwa kuwasilishwa Ofisi ya CAG kwa ukaguzi maalum. Baada ya Ukaguzi huo, Ofisi ya CAG iliwasilisha ripoti ya ukaguzi wa tofauti hiyo Wizarani na kwa Kamati ya TEITI, Novemba, 2019. Ripoti hiyo ilionesha kuwa, asilimia 90 ya tofauti imehakikiwa na kusuluuhishwa.

120. ***Mheshimiwa Spika***, Matokeo ya ukaguzi wa tofauti iliyojitokeza katika ripoti ya nane (8) ya TEITI ilisababishwa na makosa katika kutoa takwimu, kushindwa kuainisha malipo na mapato kwa usahihi na utofauti katika viwango vya kubadilisha fedha. Wakati Wizara inaendelea kufanya kazi tofauti iliyobaki, **nitoe rai kwa Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, na Taasisi za Serikali zinazohusika, kutunza nyaraka na takwimu zao kwa umakini na weledi mkubwa ili kuepusha kutokea kwa tofauti siku zijazo.**
121. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Kifungu cha 16(1) (b) cha Sheria ya TEITA 2015, tarehe 31 Desemba, 2019 TEITI iliweka wazi taarifa za wamiliki wa hisa za kampuni 37 za Madini, Mafuta na Gesi Asilia katika Tovuti ya TEITI. Lengo la kuweka wazi taarifa hizo ni: Kuimarisha uwazi katika umiliki wa

Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia; na kupunguza mianya ya rushwa pamoja na ukwepaji wa kodi. Kazi hii ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali iliyotolewa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa mapambano dhidi ya rushwa uliofanyika London Mei, 2016 (London Anti-Corruption Summit). Aidha, hatua inayofuata kwa sasa ni uanzishaji wa rejestra itakayoweka wazi taarifa za wamiliki wa hisa katika kampuni hapa nchini.

122. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi ya takwimu zinazopatikana katika ripoti za TEITI pamoja na kuitangaza TEITI na majukumu yake, TEITI iliendesha vipindi kupitia vituo vya runinga vya TBC, Channel ten na Azam. Vipindi hivyo vililenga kuhamasisha matumizi ya takwimu zinazotolewa na kuibua mijadala kwa ajili ya kuboresha na kuhamasisha uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

v. Chuo cha Madini

123. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Madini ni Taasisi chini ya Wizara ya Madini yenye jukumu la kutoa mafunzo ya Ufundu Mchundo (Technicians) kwa ngazi ya Cheti na Stashahada (Diploma). Chuo kina kampasi

mbili za Dodoma na Nzega. Mafunzo yanayotolewa ni ya muda mrefu, mfupi na mafunzo maalum yanayoandaliwa kulingana na mahitaji ya wadau (tailor made courses).

124. **Mheshimiwa Spika**, kozi zinazofundishwa katika Chuo cha Madini ni pamoja na: Jiolojia na Utafutaji wa Madini; Sayansi za mafuta na Gesi; Uhandisi Uchimbaji Madini; Uhandisi Uchenjuaji Madini; Uhandisi na Usimamizi wa mazingira Migodini; na Upimaji Ardhi na Migodi. Mafunzo hayo yanatolewa kwa njia ya umahiri (Competency Based Education Training). Katika kipindi rejewa Chuo kimetekeleza majukumu yafuatayo: -
- (a) **Kutoa Mafunzo ya Kada ya Ufundis Mchundo Katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

125. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa masomo wa 2019/2020, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 548 waliodahiliwa katika fani za Madini, Mafuta na Gesi asilia. Wanafunzi 85 wamedahiliwa katika fani ya Jiolojia na Utafutaji madini; 98 katika Uhandisi Uchimbaji Madini; 115 katika Uhandisi Uchenjuaji Madini; 42 katika Uhandisi na Usimamizi wa mazingira Migodini; 72 katika Sayansi za Mafuta na Gesi; na 136 katika

Upimaji wa Ardhi na Migodi. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 70 kutoka katika migodi mikubwa, midogo na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika fani za uchorongaji na ulipuaji wa miamba, uchenjuaji na utafutaji wa madini.

126. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Masomo 2019/2020, jumla ya wanafunzi 100 wamehitimu mafunzo katika fani mbalimbali kwa ngazi ya Stashahada (Diploma).



Picha Na. 22: Wanafunzi wa Chuo cha Madini wakifanya mafunzo kwa vitendo mgodini.

(b) Kufanya Tafiti na Kutoa Ushauri Elekezi

127. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kimeendelea kuboresha namna ya kufanya tafiti na utoaji wa ushauri elekezi. Katika maboresho hayo, Chuo kimekamilisha Sera ya Chuo ya Utafiti na Ushauri Elekezi; na Mwongozo wa Mafunzo ya Uchorongaji na Ulipuaji wa Miamba pamoja na kuwawezesha Wakufunzi Wahandisi kufanya usajili katika Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB).

(c) Kuboresha Miundombinu ya Chuo cha Madini Kampasi ya Dodoma na Nzega

128. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi, 2020 Chuo kimeboresha miundombinu na mazingira ya kujifunzia kwa kuendelea na ujenzi wa jengo la taaluma katika Kampasi ya Dodoma na kufanya ukarabati wa majengo, mifumo ya umeme, maji safi na maji taka katika Kampasi zote mbili. Maeneo yaliyokarabatiwa ni pamoja na madarasa, mabweni, nyumba za watumishi na ofisi. Aidha, Chuo kimeendelea kuimarisha utoaji wa huduma zake kwa kuongeza vifaa vya kufundishia na vya ofisi.

(d) Kuwajengea Uwezo Watumishi

129. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Chuo kwa kushirikiana na Wizara kimewezesha watumishi ishirini (20) wa kada mbalimbali kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ndani na nje ya nchi. Watumishi kumi na sita (16) wanaendelea kupata mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Aidha, Chuo kimefanikiwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mfupi ya kujiandaa kustaaafu watumishi wake 4.

(e) Ukusanyaji wa Maduhuli

130. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Chuo kilikadiriwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 532,610,000.00**. Hadi kufikia Machi, 2020, Chuo kilikuwa kimekusanya jumla ya **shilingi 225,380,000.00** sawa na **asilimia 70.5** ya lengo kwa kipindi husika. Makusanyo haya yalitokana na ada ya mafunzo, usajili na malazi.

(f) Chuo cha Madini kulelewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

131. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya Wizara kubaini uwepo wa changamoto za kitaaluma katika Chuo cha Madini, iliona kuna uhitaji wa Chuo hicho kulelewa na Chuo Kikuu chenye uzoefu wa kufanya ulezi wa vyuvo vyta namna hii hapa nchini. Lengo la Wizara kuomba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kukilea Chuo cha Madini ni pamoja na: Kuongeza nafasi za udahili katika Chuo cha Madini; kukiwezesha Chuo cha Madini kuendesha programu zinazoendana na uhitaji wa soko la ajira; kuongeza ufanisi katika maeneo muhimu ya utafiti na uchapishaji; na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa na Chuo cha Madini.



Picha Na.23: Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo-Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa pamoja wakitia saini hati ya makubaliano (MoU) kuhusu Chuo cha Madini kulelewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

132. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, hati ya makubaliano kati ya Wizara na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya namna ya kukilea Chuo imekamilika na kusainiwa. Kwa sasa hatua inayofuata ni ukamilishwaji wa Sheria ya kuanzishwa kwa Chuo, Muundo pamoja na Miundo ya Kiutumishi.

vi. Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC)

133. ***Mheshimiwa Spika***, majukumu ya Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC) ni pamoja na: kutoa mafunzo kwa ngazi ya Cheti na Stashahada (Diploma) katika fani ya teknolojia ya madini na usonara (*gem and jewellery technology*); kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za *gemmology, gem identification, synthetic and treated gem identification, coloured gem grading and pricing, diamond grading and pricing, lapidary, gem and rock carving, jewellery design and manufacturing*; kutoa huduma za kusanifu madini ya vito na miamba; kutoa huduma za kimaabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara kwa kutoa vyeti vya uthibitisho (Certificate of Authenticity); utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo, ushauri elekezi; kufanya tafiti za kuyaongezea thamani madini; na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini. Katika kipindi rejewa Kituo kimefanya yafuatayo: -

(a) Kuendelea Kutoa Mafunzo kwa Ngazi ya Cheti katika Fani za Teknolojia ya Madini na Usonara

134. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi rejewa, Kituo kimedahili wanafunzi 36 kwa Mafunzo ya Muda Mrefu katika ngazi ya Cheti (NTA Level 4) katika fani ya Teknolojia ya Madini na

Usonara. Udhili huo ni sawa na ongezekezo la asilimia 111.7 ikilinganishwa na wanafunzi 17 kwa Mwaka 2018/2019 na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi 53 wanaoendelea na mafunzo hayo. Aidha, wanafunzi 39 walidahiliwa kujiunga na mafunzo ya muda mfupi (miezi sita na mitatu) katika fani za utambuzi wa madini ya vito, ukataji na ung'arishaji madini ya vito ambao kati ya hao wanafunzi 11 walihitimu mafunzo na wengine wanaendelea na masomo hayo.



Picha Na. 24: Wanafunzi wa Kituo cha TGC wakiwa katika mafunzo ya uongezaji thamani madini

135. **Mheshimiwa Spika**, wanafunzi 17 katika teknolojia ya vito na usonara walihudhuria mafunzo ya ugani kwa muda wa wiki nane (8) katika ofisi za madini za mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Shinyanga, Mirerani-Manyara, mgodi wa Williamson Diamond Limited - Shinyanga na Arusha Gemological Laboratory. Aidha, wanafunzi wa fani ya ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito walihudhuria mafunzo ya ugani kwa muda wa wiki nne katika kampuni zinazojishughulisha na uongezaji thamani madini ya vito jijini Arusha, Dar es Salaam na Mirerani Mkoa wa Manyara.

(b) Kutoa Huduma kwa Wadau wa Madini

136. **Mheshimiwa Spika**, Kituo kiliendelea kutoa huduma mbalimbali za uongezaji thamani madini kwa wadau ikiwa ni pamoja na utambuzi wa madini ya vito, usanifu madini ya vito, uchongaji wa vinyago vya miamba pamoja na *gemstone tumbling* kwa wadau. Aidha, Taasisi za Serikali zimeanza kutumia bidhaa zinazozalishwa kituoni ikiwa ni kielelezo cha mwitikio wa kuthamini bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.



Picha 25: Vinyago Vilivyotengenezwa kwa mawe na Kituo cha TGC Arusha kwa ajili ya Mapambo ya Nyumbani na Ofisini

(c) Kuwajengea uwezo watumishi

137. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imepeleka nchini India wakufunzi wawili (2) ili kuwaongezea ujuzi katika masuala ya jimolojia na usonara. Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Kituo hicho kulingana na mahitaji na upatikanaji wa fedha.

D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

138. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2015-2030; Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2019/2020 – 2023/2024; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti wa Mwaka 2020/2021; Maagizo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliyoyatoa katika nyakati tofauti; na ushauri na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa nyakati tofauti.
139. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/21, Wizara imejiwekea maeneo yafuatayo ya kipaumbele:- kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na Rasilimali Madini; kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini na kuweka mazingira bora yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija; kuendelea

kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi na kukusanya takwimu za madini.

140. **Mheshimiwa Spika**, vipaumbele vingine ni pamoja na kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo; kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini; kuendelea kuweka mikakati ya kuimarisha soko la Tanzanite na madini mengine ya vito; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Wizara; kuimarisha shughuli za kitafiti za kijiosayansi; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.
- i. **Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na Rasilimali Madini**
141. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2020/2021, Wizara inapanga kukusanya jumla ya **shilingi 547,735,863,597** ikilinganishwa na **shilingi 476,380,613,492** kwa mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 14.98**. Kati ya fedha zitakazokusanywa, **shilingi 526,722,547,000** sawa na **asilimia 96.16** zitawasilishwa Hazina na **shilingi 21,013,316,597** sawa na **asilimia**

3.84 zitatumika na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

ii. **Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini na kuweka mazingira bora yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini**

142. **Mheshimiwa Spika**, katika kipaumbele hiki Wizara itafanya yafuatayo: kukagua na kufuatilia utekelezaji wa kanuni za usalama, afya na mazingira na kurekebisha kasoro zitakazojitokeza ili kuwa na uchimbaji madini endelevu; kuhakikisha migodi inaweka Hati Fungani ya Uhifadhi wa Mazingira na Mpango wa Ufungaji Migodi; kukagua na kuhakiki kiasi na ubora wa madini yanayozalishwa; kuongeza ushiriki wa Serikali katika uwekezaji kwa kuhakikisha migodi ya kati na mikubwa *itakayoanzishwa* inatoa *free carried interest* isiyopungua asilimia 16 na kuzisimamia ili kuhakikisha matarajio ya nchi kutokana na uwekezaji huo yanafikiwa; kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ya madini kwa kushirikiana na sekta binafsi; na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini katika shughuli za utafiti na uchimbaji madini.

iii. Kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija

143. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini Wizara itafanya yafuatayo:- kuendelea kutenga maeneo yanayofaa kwa Wachimbaji Wadogo; kuwapa elimu kuhusu uwepo na faida za kuuza madini yao katika masoko yaliyoanzishwa; kutoa huduma nafuu za kitaalam kwa Wachimbaji Wadogo ikiwa ni pamoja na kuwafahamisha kuhusu uwepo wa mashapo katika maeneo yaliyobainishwa na kutengwa kwa ajili yao; na kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini yenye tija na namna ya kupata mikopo kutoka kwenye Taasisi za fedha.

iv. Kuendelea kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi na kukusanya takwimu za madini

144. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi na kukusanya takwimu za madini kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali, Wizara itafanya yafuatayo:- kuimarisha ukaguzi wa migodi mikubwa na ya kati ili kupata taarifa sahihi za uwekezaji, uzalishaji, na mauzo kwa lengo la kuhakikisha tozo na kodi mbalimbali za

Serikali zinatozwa kwa usahihi; kuhakikisha kila mgodi mkubwa, wa kati na maeneo ya wachimbaji wadogo unakuwa na Afisa Mgodi Mkazi ili kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi za uzalishaji kwa lengo la kutoza tozo stahiki; kufuatilia taarifa za ununuzi na uuzaji (returns) kwa wafanyabiashara wa madini (Dealers & Brokers).

145. ***Mheshimiwa Spika***, shughuli nyingine ni pamoja na kusimamia Sheria katika kukuza ushiriki wa nchi na wananchi (local content) katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini; kufuatilia uwajibikaji wa Kampuni za uchimbaji madini kwa jamii (Corporate Social Responsibility); kuimarisha ukaguzi wa madini ya ujenzi na viwandani; kufuatilia wadaiwa wa tozo mbalimbali za madini kwa mujibu wa Sheria kwa wakati; kudhibiti uchimbaji na uchenjuanji haramu wa madini; na kuboresha na kuimarisha Mfumo wa kutoa leseni za madini na kutunza taarifa zake.
- v. **Kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo**
146. ***Mheshimiwa Spika***, ili kufikia azma ya kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya

yafuatayo:- kuweka vifaa muhimu nya upimaji wa madini katika masoko hayo; kuhakikisha kuwa huduma zote za msingi ikiwemo za kifedha na mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato mbalimbali zinakuwepo ili kuwaondolea usumbufu wauzaji na wanunuzi wa madini; kuimarisha usalama; kuhakikisha uwepo wa wataalamu wa kutosha katika masoko; na kuanzisha masoko mapya kulingana na mahitaji.

vi. Kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini

147. ***Mheshimiwa Spika***, katika kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:-kuendelea kuimarisha usimamizi katika maeneo yote ya uzalishaji kwenye migodi mikubwa na ya kati kwa kuwaweka Maafisa Migodi Wakazi (MROs) kusimamia na kuwasilisha taarifa za uzalishaji wa kila siku pamoja na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini; Wizara kwa kushirikiana na mamlaka husika za Serikali itahakikisha kuwa katika maeneo ya viwanja nya ndege na mipakani wanakuwepo wasimamizi ili kuhakikisha kuwa madini yanapitishwa kwa vibali husika; na Kufanya kaguzi maalum za kimkakati mara kwa mara katika maeneo ya shughuli za madini.

vii. Kuendelea kuweka mikakati ya kuimarishe soko la Tanzanite na madini mengine ya vito

148. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarishe soko la madini ya tanzanite na madini mengine ya vito Wizara itafanya yafuatayo:- kuendelea kuimarishe ulinzi katika eneo tengefu la Mirerani; kuhakikisha kuwa shughuli zote za uchimbaji na biashara ya madini ya tanzanite zinafanyika ndani ya ukuta; kuhakikisha kuwa madini ya vito yanachimbwa na wazawa kwa mujibu wa Sheria; na kuhakikisha kuwa madini ya vito yanauzwa katika masoko ya madini nchini kwa kuzingatia bei elekezi ya soko la dunia.

viii. Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

149. **Mheshimiwa Spika**, katika kukuza uwezo wa uongezaji thamani madini, Wizara itafanya yafuatayo:- kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kuchakata madini hapa nchini kama vile *Smelters* na *Refineries*; kukiimarishe Kituo cha Jimolojia Tanzania ili kiweze kutoa wataalamu bora watakaokidhi mahitaji ya soko; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini na vito (usonara na uchongaji); na kubainisha na kuhamasisha

matumizi ya madini ya viwandani katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

ix. Kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Wizara

150. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itafanya yafuatayo katika kuimarisha Taasisi zinazohusika na masuala ya madini:- kuzipatia rasilimaliwatu, fedha na vitendea kazi ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; na kuzisaidia katika kuandaa Mipango Mikakati inayoendana na Sera na Mipango ya nchi.

x. Kuimarisha shughuli za utafiti za jiosayansi

151. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itahakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufanyia tafiti; kuimarisha maabara ya GST na kuhakikisha uwepo wa vifaa na wataalam; na kuwaendeleza wataalam ili kuendana na kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia katika Sekta ya Madini.

xi. Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi

152. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi, Wizara

itaendelea kuwajengea uwezo na kuongeza ujuzi kwa watumishi katika nyanja mbalimbali; kuzuia maambukizi mapya ya Virusi vyta UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY); na kutoa huduma ya lishe kwa walioweka wazi kuwa na UKIMWI. Aidha, Wizara itaboresha mazingira ya kazi kwa kutoa vitendea kazi, kuboresha maslahi ya watumishi, kuhamasisha uadilifu na kujiepusha na vitendo vyta rushwa.

KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021

i. Tume ya Madini

153. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021 Tume ya Madini inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kusimamia biashara ya madini na masoko yaliyoanzishwa

154. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza jukumu hilo Tume ya Madini itafanya yafuatayo: kudhibiti utoroshaji wa madini; kusimamia shughuli zote za uthaminishaji madini nchini na kushiriki minada ya madini ndani na nje ya nchi; kuandaa bei elekezi; usimamizi wa shughuli za maabara; na kusimamia utekelezaji wa kanuni za

uwezeshaji wananchi kiuchumi (local content) katika Sekta ya Madini.

(b) Kuimarisha Shughuli za Ukaguzi wa Migodi na Mazingira nchini

155. **Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, Tume ya Madini itaendelea kufanya ukaguzi katika Migodi mikubwa na midogo nchini; kuendelea na vikao vya ufungaji wa migodi chini ya Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi (NMCC) kwa lengo la kuipitia Mipango ya Ufungaji migodi na kuhibitisha; pamoja na kuendelea na elimu ya ugani kuhusu usalama mahala pa kazi kwa lengo la kupunguza ajali migodini.

(c) Kuboresha shughuli za Usimamizi, utoaji wa Leseni na masuala ya TEHAMA

156. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha shughuli za TEHAMA kwa kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo (*Local Area Network-LAN*) na (*Wide Area Network-WAN*) katika Ofisi mbalimbali za madini nchini ili kurahisisha upatikanaji wa Mfumo wa Usimamizi na Utoaji wa Leseni za Madini nchini kwa urahisi zaidi.

(d) Kuendeleza Rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi

157. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021 Tume ya Madini itaendelea

kuwajengea uwezo wa kiujuzi watumishi wake katika nyanja mbalimbali kulingana na uhitaji; kuboresha mazingira ya kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana; kuendelea kutoa elimu kwa watumishi juu ya kuzuia maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa huduma ya lishe bora kwa Watumishi waliokwisha athirika; na kuhamasisha uadilifu mahali pa kazi.

(e) Uelimishaji na Uhabarishaji Umma na Usimamizi wa Masuala ya Kisheria

158. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha migogoro inapungua au kuisha kabisa katika Sekta ya Madini, Tume ya madini itaendelea kutoa elimu na huduma ya ugani juu ya masuala ya kisheria pamoja na miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Madini nchini kuitia redio, runinga, *blogs* na tovuti juu ya maendeleo ya Sekta ya Madini nchini.

ii. Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

159. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

(a) Kuboresha kanzidata ya Miamba na Madini ya Taifa ili kuongeza uelewa wa jiolojia ya nchi na kuchochea uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini

160. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha kanzidata ya miamba na madini nchini GST inakusudia kufanya; Utafiti wa jiolojia katika QDS 124, 190 na 316 na jiomeria QDS 124 na 125 zilizopo katika Mkoa wa Lindi na Dodoma kwa skeli ya 1:100,000; kufanya tafiti maalum mbili (2), kuendeleza tafiti na kuzalisha *crucible* na *cupels* 15,000; kuchora ramani 25 na *ku-scan* machapisho 1,000 kutoka katika mfumo wa karatasi na kwenda katika mfumo wa dijitali pamoja na sampuli za makumbusho (museum) 50 na kuweka kwenye *Geological Mineral Information System* (GMIS); kufanya utafiti wa jiosayansi kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia ya China (China Geological Survey).

(b) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za jiosayansi katika utafutaji, uchimbaji salama, uchenjuaji na uhifadhi wa mazingira

161. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: utafiti wa jiosayansi kwa lengo la kutambua ulalo,

muelekeo na tabia za mbale katika maeneo manne (4) ya wachimbaji wadogo yaliyopo Mkoa wa Katavi na Mara; Utafiti wa jiosayansi katika maeneo mawili (2) yatakayobainishwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

(c) Kuboresha Huduma za Maabara kwa Wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi

162. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha huduma za maabara, GST imepanga kufanya mambo yafuatayo: kufanya uchunguzi wa maabara kwa sampuli 15,000; kuendeleza programu mbalimbali za kusimamia ubora wa huduma za maabara; na kuboresha miundombinu, mitambo na vifaa vyaa maabara.

(d) Kuboresha kanzidata ya majanga ya asili ya jiolojia na kuelimisha wananchi namna bora ya kujikinga na majanga

163. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha kanzidata ya majanga ya asili ya jiolojia, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: kukusanya takwimu na kuzichakata kutoka katika vituo vyote tisa (9) na kuhuishaa ramani inayooonesha vitovu vyaa matetemeko ya ardhi nchini; kufanya utafiti wa kina wa hali ya matetemeko ya ardhi katika Mji wa Serikali; kusimika vituo viwili vipya vyaa kuratibu

matetemeko ya ardhi katika Mkoa wa Kigoma na Kagera.

(e) Kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma na ukusanyaji wa mapato

164. ***Mheshimiwa Spika***, Ili kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma na ukusanyaji wa mapato, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: kuboresha vitendea kazi na mazingira ya kazi; kuendeleza watumishi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wao; kuboresha muundo wa GST ili kuongeza ufanisi na kuboresha mtambo wa kutengeneza vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu na fedha ili uweze kuzalisha kibiasara.

iii. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

(a) Kuimarisha shughuli za uchimbaji na uzalishaji madini

165. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka wa Fedha 2020/21 Shirika linatarajia kutekeleza yafuatayo: kuongeza uzalishaji katika mradi wake wa makaa ya mawe wa Kabulo-Kiwira kwa kuongeza vifaa vya uchimbaji wa makaa ya mawe pamoja na masoko.

166. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika linatarajia pia kuongeza uzalishaji katika Kampuni ya STAMIGOLD kutoka wastani wa wakia 1,150 hadi kufikia wakia 1,500 kwa mwezi. Sambamba na hilo mgodi unatarajia kuanza utekelezaji wa mradi wa kuchenjua visusu vya dhahabu na kuimarisha shughuli za utafiti na uchorongaji ili kuongeza uhai wa mgodi.

(b) Kuanza utekelezaji wa Miradi mipya na kuimarisha shughuli za uchorongaji

167. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika pia linatarajia kuanza uzalishaji katika miradi mipya miwili ambayo ni mradi wa kusafisha dhahabu uliopo jijini Mwanza na mradi wa kuchimba dhahabu wa Buhemba. Miradi hii inatarajiwa kuanza uzalishaji Desemba, 2020. Aidha, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za kibiasara za uchorongaji na kutoa ushauri wa mazingira kwa kuongeza vifaa na wataalamu. Vilevile, Shirika linatarajia kununua mitambo mipya mitatu (3) ya uchorongaji (drilling rig).

(c) Kuendelea kuratibu na kuendeleza shughuli za wachimbaji wadogo

168. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa uratibu wa uendelezaji wa wachimbaji wadogo, Shirika litaendelea kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo katika vituo vya Katente,

Lwamgasa na Itumbi na kutoa elimu ya uchimbaji bora kwa wachimbaji wadogo nchini.

iv. Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

169. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazotekelzwa na TEITI katika Mwaka 2020/2021 zitahusisha: kukamilisha na kutoa kwa Umma ripoti ya ulinganisho wa malipo ya kodi yanayofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na mapato yaliyopokelewa na Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2018/2019; kuendelea kuelimisha Umma juu ya matumizi ya takwimu zinazotolewa katika ripoti za TEITI ili waweze kutumia takwimu hizo katika kuhoji uwajibikaji wa Serikali kwa njia ya warsha, matangazo, vipindi vya redio, runinga na makala; uwekaji wazi wa majina ya watu wanaomiliki hisa katika kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na kuweka wazi mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

v. Chuo cha Madini (MRI)

(a) Kuendelea Kutoa Mafunzo Katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia

170. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo cha Madini kinapanga

kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 548 kwa Mwaka wa Masomo 2019/20 hadi kufikia wanafunzi 750 kwa Mwaka wa Masomo 2020/2021 sawa na ongezeko la **asilimia** **36.9.** Ongezeko hili litapelekea kufikia lengo la Mpango Mkakati wa Chuo wa kuwa na wanafunzi 1,000 ifikapo mwaka 2022.

(b) Kuendelea Kuboresha Miundombinu ya Chuo

171. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo cha Madini kitaendelea kukarabati miundombinu katika Kampasi za Dodoma na Nzega kama vile; mabweni ya wanafunzi, madarasa, maabara, nyumba za watumishi pamoja na miundombinu mingine ya maji na umeme. Aidha, Chuo kitaendeleza na kusimamia upatikanaji wa mawasiliano chuoni (ICT) ili kukidhi mahitaji yatokanayo na ongezeko la wanafunzi na watumishi; kuongeza vitendea kazi kama vile vifaa vya ofisi, maabara, vifaa vya kufundishia pamoja na vitabu.

(c) Kuwajengea Uwezo Watumishi

172. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo kitaendelea kuwajengea uwezo watumishi wa kada zote kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi ili kuwapa utalaam na ujuzi

utakaowaongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

(d) Kuendelea Kufanya Tafiti na Kutoa Ushauri Elekezi

173. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo cha Madini chini ya ulezi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kitaendelea kufanya tafiti katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, kutoa ushauri elekezi (consultancy) katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia; pamoja na kuwasilisha maandiko juu ya kazi za kitafiti katika majarida mbalimbali ya kisayansi kwa ajili ya uchapishaji.

vi. Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC)

(a) Kutoa Mafunzo na Uzalishaji

174. **Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Jimolojia Tanzania pamoja na majukumu mengine kitatekeleza yafuatayo:- kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi ya Cheti na Stashahada katika fani ya Teknolojia ya Madini na Usonara (Gem and Jewellery Technology); kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za gemmology, gem identification, synthetic and treated gem identification, coloured gem grading and pricing and diamond

grading and pricing, lapidary, gem and rock carving, jewellery design and manufacturing; kutoa huduma za kusanifu madini ya vito na miamba; kutoa huduma za kimaabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara kwa kutoa vyeti vya uthibitisho (Certificate of Authenticity); utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo (usonara); kutoa ushauri na ugani kwa wadau wa madini; kufanya tafiti za kuyaongeza thamani madini; na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini.

(b) Kukijengea uwezo Kituo

175. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatarajia kuwaendeleza kielimu watumishi wanne (4) katika vyuvo vilivyobobea katika masuala ya uongezaji thamani madini. Aidha, Wizara imepanga kuajiri watumishi katika kada mbalimbali ambao watakuwa wakufunzi katika Kituo cha Jimolojia Tanzania.

E. SHUKRANI

176. **Mheshimiwa Spika**, nakiri kuwa azma ya Taifa letu ya kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025, inaendelea kutupa hamasa ya kufanya kazi kwa juhudzi zaidi. Hamasa hii inatokana na juhudzi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza sekta mbalimbali za uzalishaji ikiwemo Sekta ya Madini ninayoisimamia. Kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuliongoza Taifa letu na kuwaletea watanzania maendeleo ya kweli yanayoonekana kwa vitendo.

177. **Mheshimiwa Spika**, ninamuomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema amjalie Mheshimiwa Rais afya njema ili aendelee kutekeleza majukumu yake na kutimiza ndoto na maono yake ya kulifikisha Taifa hili katika Uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda na usimamizi thabiti wa utekelezaji wa ahadi za Ilani ya CCM.
178. **Mheshimiwa Spika**, ninaombra nitumie nafasi hii tena kuwashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo yao wanayotupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu. Aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, nimshukuru pia Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.), Naibu Waziri

wa Madini kwa namna anavyonipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini.

179. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Prof. Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru, Mhandisi David Mulabwa, Kamishna wa Madini, Prof. Idris Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Meja Jenerali (Mstaafu) Michael Isamuhyo, Mwenyekiti wa Bodi ya STAMICO, Prof. Justinian Ikingura, Mwenyekiti wa Bodi ya GST, Bw. Ludovick Utouh Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI, Prof. Hudson Nkotagu, Mwenyekiti wa Bodi ya MRI, Makamishina wa Tume na wajumbe wa Bodi zote kwa kusimamia kwa umakini uendeshaji wa Sekta ya Madini.
180. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, ninawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha kuwa majukumu ya Wizara ya Madini yanatimizwa ipasavyo na hivyo kuifanya Sekta ya Madini kuzidi kuimarika na kwenda mbele.

181. **Mheshimiwa Spika**, niendelee kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa ushirikiano wao ambao kwa namna moja au nyingine umeiwezesha Wizara kufikia malengo yake. Nipende kuwatambua kwa kuwataja baadhi yao kama ifuatavyo: Benki ya Dunia; Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Watu wa Korea ya Kusini, Misri, Australia na JOGMEC. Aidha, nazishukuru pia Taasisi, Mamlaka mbalimbali na Wadau wa Sekta ya Madini ambao wamesaidiana na Wizara katika masuala mbalimbali. Kipekee niwashukuru Uongozi Institute na REPOA kwa kutujengea uwezo katika masuala ya Uongozi na uandaaji wa Sera. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika ikuendeleza Sekta.
182. **Mheshimiwa Spika**, shukrani zangu za pekee na za dhati pia naomba nizitoe tena kwa wananchi wema, watu wa kusema na kutenda wa jimbo la Bukombe ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na kitaifa na wakati mwingine kunivumilia kwa kukosa huduma yangu nilipokuwa nikitekeleza majukumu ya kitaifa. Napenda kuwaahidi na kuwahakikishia kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote kwa kipaji alichonipa mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

Naomba ushirikiano huu udumu ili kwa pamoja tuendelee kujenga Bukombe yetu.

183. **Mheshimiwa Spika**, napenda kipekee kabisa kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Benadetha Clement Mathayo pamoja na watoto wetu Elshadai, Elvin, Elis, Abigael, Amon, Abishai na Moses kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu.

F. HITIMISHO

184. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu ya Wizara ya Madini katika Mwaka 2020/2021, naomba Bunge lako Tukufu sasa liridhie na kupitisha makadirio ya Jumla ya **shilingi 62,781,586,000** kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na Taasisi zake. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Bajeti ya Maendeleo ni **shilingi 8,500,000,000.** ambazo zote ni fedha za ndani; na
- (ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni **shilingi 54,281,586,000.** ambapo **shilingi 21,045,927,000.** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi**

33,235,659,000 ni Matumizi
Mengineyo (OC).

185. **Mheshimiwa Spika**, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Kwa kuwa hili ni Bunge la mwisho kuelekea Uchaguzi Mkuu, naomba nichukue nafasi hii kuwatakiia uchaguzi mwema. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.madini.go.tz. Vilevile, hotuba hii ina majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini.
186. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

VIAMBATANISHO

**VIELELEZO VYA HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA MADINI KWA MWAKA
2020/2021**

Jedwali Na. 1: Makadirio na Makusanyo Halisi ya Maduhuli kwa Kila Kituo kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na Makadirio kwa Mwaka 2020/2021

Na.	MKOA / KITUO CHA MAKUSANYO	Malengo ya makusanyo 2019/20	Makusanyo Halisi kufikia Machi, 2020	Asilimia ya makusanyo 2019/20	Malengo ya Makusanyo 2020/21
1.	Makao Makuu	26,049,500,000	14,028,776,575	54	20,000,000,000
2.	RMO - Arusha	3,789,250,000	3,383,854,133	89	4,000,000,000
3.	RMO - Chunya	18,860,500,000	29,115,592,889	154	22,069,875,383
4.	RMO - Dodoma	2,800,000,000	1,889,310,817	67	3,000,000,000
5.	RMO - Dsm	13,157,000,000	8,776,798,706	67	11,500,000,000
6.	RMO - Geita	156,349,687,500	150,613,815,725	96	200,000,000,000
7.	RMO - Kagera	3,500,000,000	2,493,125,315	71	4,017,403,331
8.	RMO - Kahama	78,785,000,000	41,092,140,873	52	79,000,000,000
9.	RMO - Katavi	1,000,000,000	1,350,699,615	135	1,250,000,000
10.	RMO - Kigoma	1,000,000,000	252,009,912	25	1,000,000,000
11.	RMO - Kilimanjaro	1,500,000,000	889,324,258	59	1,500,000,000
12.	RMO - Lindi	2,000,000,000	1,134,052,120	57	2,000,000,000
13.	RMO - Manyara	1,000,000,000	504,264,834	50	1,000,000,000
14.	RMO - Mara	103,099,000,000	67,750,449,416	66	108,024,000,000
15.	RMO - Mbeya	8,875,000,000	1,650,371,413	19	1,500,000,000
16.	RMO - Mirelani	6,389,250,000	1,925,302,378	30	4,000,000,000
17.	RMO - Morogoro	2,200,000,000	1,162,931,823	53	1,893,675,000
18.	RMO - Mtwara	3,010,000,000	1,467,926,334	49	2,100,000,000
19.	RMO - Mwanza	3,000,000,000	3,047,140,700	102	3,600,000,000
20.	RMO - Njombe	1,515,700,000	328,152,854	22	1,000,000,000
21.	RMO - Rukwa	1,000,000,000	266,800,522	27	1,000,000,000
22.	RMO - Ruvuma	5,043,960,000	5,382,576,939	107	7,564,500,000
23.	RMO - Shinyanga	18,157,000,000	12,545,928,231	69	18,200,000,000
24.	RMO - Simiyu	200,000,000	109,544,654	55	250,000,000
25.	RMO - Singida	1,500,000,000	3,243,231,675	216	3,000,000,000
26.	RMO - Tabora	2,273,550,000	2,525,176,234	111	2,500,000,000
27.	RMO - Tanga	4,300,000,000	1,589,645,419	37	3,500,000,000
28.	RMO- Iringa	0	124,926,435	0	750,000,000
29.	RMO- Songwe	0	0	0	17,503,091,701
JUMLA		470,354,397,500	358,643,870,797	76	526,722,545,415

Jedwali Na. 2: Kiasi cha Mrabaha na ada ya ukaguzi kilichokusanywa kutoka kwenye madini mbalimbali kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi Februari, 2020

N a	Aina ya Madini	Kizio cha Uzito	Uzito	Thamani (TZS)	Mrabaha (TZS)	Ada ya Ukaguzi (TZS)	Makusanyo (TZS)	
1	Dhababu (wachimbaji wa kubwa na Katii)		Kg	25,435	2,772,331,030,318	166,339,861,819	27,723,310,303	194,063,172,122
2	Dhababu (wachimbaji wadogo)		Kg	10,102	975,430,320,905	58,525,819,254	9,754,303,209	68,280,122,463
3	Fedha		Kg	8,468	10,696,760,115	641,805,607	106,967,601	748,773,208
4	Almasi		Karati	210,228	89,850,459,114	5,391,027,547	898,504,591	6,289,532,138
5	Tanzanite (Rough)		Kg	3,799	22,593,302,710	1,339,449,477	227,298,854	1,566,748,331
6	Tanzanite (Cut and Polished)		Karati	94,135	28,057,959,661	286,263,678	284,834,430	571,098,108
7	Tanzanite (Beads)		Kg	26,344	2,133,618,627	128,017,331	21,336,413	149,353,744
8	Kinywe (Graphite)		Tani	7,146	7,748,668,420	232,460,053	77,486,684	309,946,737
9	Makaa ya mawe		Tani	434,485	89,082,581,845	2,672,477,455	890,825,818	3,563,303,274
10	Madini mengineyo ya vito		Kg	1,120,66 6	33,411,433,004	2,004,685,980	334,114,330	2,338,800,310
11	Madini ujenzi		Tani	22,036,0 69	265,291,911,850	7,958,757,355	2,652,919,119	10,611,676,474
12	Madini ya viwandani		Tani	951,773	34,022,968,857	1,020,689,066	298,972,048	1,319,661,114
13	Madini mengineyo		Tani	196,864	20,166,039,175	646,977,443	201,660,392	848,637,834
TOTAL				4,350,817,054,601	247,188,292,065	43,472,533,792	290,660,825,857	

Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Mauzo na Mapato ya Dhahabu katika Masoko ya Geita Chunya na Kahama kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2019 hadi Machi 2020

SOKO LA MADINI GEITA					
Mwezi	Kiasi (Kg)	Thamani (TZS)	Mrabaha (TZS)	Ada ya Ulaguzi (TZS)	Jumla ya Mapato (TZS)
Julai, 2019	328.3	29,546,427,324.24	1,772,785,639.45	295,460,232.24	2,068,245,871.69
Agosti, 2019	504.95	52,250,475,708.10	3,135,028,542.49	522,504,757.08	3,657,533,299.57
Septemba, 2019	489.8	47,647,437,459.20	2,858,846,247.55	476,474,374.59	3,335,320,622.14
Oktoba, 2019	537.61	51,808,980,677.37	3,108,538,840.64	518,089,806.77	3,626,628,647.42
Novemba, 2019	479.59	44,978,955,449.10	2,698,737,326.95	449,789,554.49	3,148,526,881.44
Disemba, 2019	457.64	43,410,671,123.85	2,604,640,267.49	434,106,711.25	3,038,746,978.74
Januari, 2020	371.61	37,095,989,241.83	2,225,759,354.51	370,959,892.42	2,596,719,246.93
Februari, 2020	348.47	34,092,412,748.26	2,045,544,764.90	340,924,127.48	2,386,468,892.38
Machi 2020	390.53	40,752,390,224.56	2,445,143,413.47	407,523,902.25	122,257,170.67
Jumla	3,908.50	381,583,739,956.51	22,895,024,397.45	3,815,833,358.57	23,980,447,610.98

SOKO LA MADINI CHUNYA

Mwezi	Kiasi (Kg)	Thamani (TZS)	Mrabaha (TZS)	Ada ya Ulaguzi (TZS)	Jumla ya Mapato (TZS)
Julai, 2019	128.75097	11,799,872,269.73	707,992,336.18	117,998,722.69	825,991,058.87
Agosti, 2019	180.51238	17,536,072,171.46	1,052,164,330.30	175,360,722.08	1,227,525,052.38
Septemba, 2019	229.98814	22,564,166,049.88	1,353,849,963.01	225,641,660.51	1,579,491,623.52
Oktoba, 2019	237.1397	23,018,877,443.45	1,381,132,646.57	230,188,774.44	1,611,321,421.01
Novemba, 2019	219.43204	21,016,907,669.19	1,261,014,460.16	210,169,076.68	1,471,183,536.84
Disemba, 2019	198.25082	18,927,954,113.19	1,135,677,246.77	189,279,541.11	1,324,956,787.88
Januari, 2020	166.69075	16,814,928,102.42	1,008,895,686.15	168,149,281.04	1,177,044,967.19
Februari, 2020	152.46608	15,972,187,769.95	958,331,268.39	159,721,875.63	1,118,053,144.02
Machi, 2020	122.16	12,762,315,975.00	765,738,959.00	127,623,161.00	38,286,947.93
Jumla	1,635.39	160,413,281,564.27	9,624,796,896.53	1,604,132,815.18	10,373,854,539.64

SOKO LA MADINI KAHAMA

Mwezi	Kiasi (Kg)	Thamani (TZS)	Mrabaha (TZS)	Ada ya Ulaguzi (TZS)	Jumla ya Mapato (TZS)
Julai, 2019	15.23824	2,486,272,103.49	149,176,326.21	24,862,721.03	174,039,047.24
Agosti, 2019	311.76066	25,130,292,344.91	1,507,817,540.69	251,302,923.45	1,759,120,464.14
Septemba, 2019	306.16955	28,165,468,470.03	1,708,384,761.77	281,654,684.70	1,990,039,446.47
Oktoba, 2019	342.75799	30,981,233,105.77	1,842,445,513.79	307,159,432.30	2,149,604,946.09
Novemba, 2019	268.51269	23,550,007,493.61	1,413,000,449.62	198,738,057.36	1,611,738,506.98
Disemba, 2019	249.34479	13,760,166,638.86	825,609,998.33	137,601,666.39	963,211,664.72
Januari, 2020	102.68056	9,926,459,240.46	595,587,554.43	99,264,592.40	694,852,146.83
Februari, 2020	95.61	9,508,701,799.03	570,522,107.94	95,087,017.99	665,609,125.93
Machi, 2020	172.57	17,119,721,646.46	1,027,183,298.59	171,197,216.49	112,092.39
Jumla	1,864.64	160,628,322,842.62	9,639,727,551.37	1,566,868,312.11	10,008,327,440.79

Jedwali Na. 4: Takwimu za Mitambo ya Uchenjuaji Dhahabu (Elutions) Nchini mpaka Machi 2020

Na		Mahali	Inayofanya Kazi	Iliyosimama	Hatua ya Ujenzi	Hatua za Majaribio	Jumla
1.	Mara	Musoma	13	-	2	-	15
		Tarime	2	-	1	-	3
2.	Kahama	Kahama	11	02	01	02	16
3.	Songwe	Chunya	24	2	8	3	37
4.	Geita	Geita	21	6	2	-	29
		Bukombe	1	-	-	-	1
		Nyang'wale	2	-	-	-	2
		Chato	2	-	-	-	2
		Mbogwe	2	-	-	-	2
5.	Shinyanga	Shinyanga	5	1	1	1	8
6.	Singida	Singida	5	2	-	-	7
7.	Tanga	Tanga	1	-	1	-	2
8.	Mwanza	Mwanza	5	-	1	-	6
9.	Dodoma	Dodoma	3	-	-	-	3
10.	Morogoro	Morogoro	1	-	-	-	1
11.	Lindi	Lindi	1	-	1	-	2
12.	Tabora	Tabora	6	-	1	-	7
13.	Mbeya	Mbeya	0	4	-	-	4
14.	Iringa	Iringa	1	1	-	-	2
15.	Manyara	Babati	1	-	-	-	1
16.	Simiyu	Simiyu	-	-	-	-	-
17.	Katavi	Mpanda	1	-	-	-	1
	Jumla		108	18	19	6	151


Jedwali Na. 5: Takwimu za maendeleo ya Taaluma kwa Wahitimu wa Mwaka wa Masomo 2018/19 katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI)

Na.	AINA YA KOZI	NTA Level 4 (2016/2017)	NTA Level 5 (2017/2018)	NTA Level 6 (2018/2019)
1.	Geology and Mineral Exploration	43	28	16
2.	Petroleum Geosciences	49	34	25
3.	Mining Engineering	37	26	15
4.	Mineral Processing Engineering	52	37	27
5.	Env. Eng. and Management in Mines	29	21	17
Jumla		210	146	100


Jedwali na 6: Matetemeko makubwa yaliyotokea kwa kipindi cha kuanzia Jualai, 2019 hadi Machi 2020

Tarehe	Muda	Mahali	Ukubwa (Richter)
30/7/2019	12:35:37 Asubuhi	Ngulu - Tabora	4.5
20/8/2019	3:54:56 Asubuhi	Naberera - Manyara	4.6
9/9/2019	9:38:44 Usiku	Sibwesa - Katavi	5.5
13/3/2020	10.55 asubuhi	Vulaya-Mpakani mwa Korogwe na Lushoto	4.9


Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020




Kielelezo Na. 2: Makusanyo ya maduhuli kwa vyanzo mbalimbali kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020



Kielelezo Na.3: Kiasi cha dhahabu kilichoalishwa katika migodi mikubwa na kuuzwa nje ya nchi, mwaka 2013 - 2019




Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Madini ya Dhahabu katika Soko la Dunia kuanzia mwaka 2007 - 2019



Chanzo: London Bullion Market Association (LBMA)

Kielelezo Na.5: Ramani inayoonesha vituo vya kupimia mitetemo ya ardhi





Mheshiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Naibu Waziri wa Madini akikagua Madini ya Bati katika Soko la Madini Kyerwa - Kagera

